# PROGRAMU YA KUSOMESHA MISINGI YA UISLAMU KWA MUISLAMU MPYA

( منهج تعليم المهتدين الجدد مبادئ الإسلام باللغة السواحيلية )

Mtunzi

Dr. AHMAD BIN MUHAMMAD AL U'BAYD

Ir. SULEYMAN BIN AHMAD AL YAHYA

Chapa nyipya

Dhul hijja 1443H/July 2022M


بسم الله الرحمن الرحيم

## *Mazungumzo hasa kwa ajili ya mwalimu na msimamizi*

**Tunawashukuru sana enyi waalimu na wasimamizi kwa kusimamia jambo hili muhimu, na tunamuomba Allah kwetu sote utakaso (ikhlas) katika kauli na vitendo, na tunakukumbusheni baadhi ya mambo, miongoni mwayo ni:**

1 ni juu lako kumuhimidi Allah na kumshukuru yeye kwa yale aliyo kuchaguwa kwayo na kukufadhilisha kwa kule kusimamia kazi ya mitume, nayo nikule kuwafundisha watu na kuwapa muono kwa yale mambo ya dini yao kwa hali ya kuwahurumiya; Amesema Mtume juu lake rehma na amani: "Kwa hakika wanachuoni ndio warithi wamanabii".

2 Na iwe nembo (alama) yako kumcha Allah aliye takasika, na uwe kiigizo chema hasa katika:

Uchangamfu na tabia njema, na upole kwa mwanafunzi, na ukweli, na muonekano mzuri, na uvumilivu na usishtushwe na kuchoka kwa uzito wa kukabiliana na baadhi ya hali za wanafunzi, na uwe kiigizo chema katika ibada mbili swala na udhu na uwe mwenye kushikamana vyema na sunna na mwenye kutekeleza vyema udhu mwenye kuharakia kutekeleza swala, kwa kuwa wanafunzi ni wenye kufatilia Zaidi mambo yako na wanakuwa ni wenye kukuiga.

3 Na ujibu kwa kusema sijuwi ikiwa wewe hauna uhakika na **jibu kuwa ni sahihi, na hasa katika mambo yenye kutatanisha**(shub-ha).

4 na uwe na daftari ya kuwa nasajili (naandika) maswali ya waisilamu wapya; ili uweze kuwafaidisha zaidi baada ya wewe kuyafanyia uchunguzi Zaidi na kuuliza kwa wengine ikiwa wewe hauyafahamu.

5 Kujihimiza sana na wale wanafunzi wanao jitahidi katika kusoma kwao na kuandika majina yao na unuwani zao ; kwa ajili ya kuwapa motisha ya kuendelea kujifunza dini yao zitakapo fanyika daurat za kielemu.

6 Na katika yale yanayo musaidia muisilamu mpya kuweza kuhifadhi nyiradi (zhikri) za baada ya swala na nyiradi za asubuhi na jioni: inapendeza kwa wanafunzi watakapo kuwa darasani tu waweze kuzirejelea rejela hizo nyiradi, na wanafunzi waweze kusimamia jambo hilo kwa kupeana zamu. (kurejelea rejelea kwa pamoja huko ifanyike wakati wamasomo basi, na wala haijuzu kurejelea rejelea kwa pamoja baada ya swala, lakini utanoma azhkaar baada ya swala asubuhi na jioni kila mmoja kivyake).

7. Iliyo kuwa bora ni mwanafunzi kuhifadhi nguzo za uisilamu na Imani kwa lugha ya kiarabu; zaidi ya hayo, nikwake kuzielewa nguzo hizo kwa lugha yake; na huko kutapelekea kwa yule aliye silimu kuhisi athari za nguzo hizo baada ya kozi (semina), na itapelekea kuimarisha Imani yake katika uislamu wake na kujinasibisha kwake kwenye usilamu na mazungumzo yake na watu.

8. Na iwe katika majukumu yako kumjenga kila mwanafunzi kuwa na mapenzi na huruma kwa watu, na awe mwenye kuharakia kutenda kila kitendo kizuri,na awe najihimiza sana kuwaita watu kwenye usilamu, na mwenye kukimbilia kutenda kila wema na kitendo kizuri.

**Zinduo:**

**Kila aliye silimu afanye yale anayo yaweza ili aweze kujua twahara(usafi),na asali sala kwa kukamilisha nguzo zake na arejelee rejelee kwa kila nguzo neno (SUB-HAANALLAH) mpaka pale atakapo jifunza nyiradi za nguzo ya swala, na ufafanuzi wake utakuja kwenye somo la tatu na la nne.**

**Tukimuomba Allah mkarimu katika fadhila zake aweze kuwawezesheni na kuwalipeni na akupeni nyote ikhlas katika kauli na vitendo**

Na programu hii inakusanya yale mambo muhimu zaidi ya misingi ya dini ya kweli ya uisilamu.

**Na program hii imegawanyika katika visomo makumi mbili (20),** ina kusanyika mafundisho ya suratul faatiha na baadhi ya sura fupi fupi na utambulisho mfupi wa qur'an tukufu, na mambo muhimu sana katika Imani (aqidah), na hadith na baadhi ya nyiradi (zhikri), na ufupi wa fiqhi ya ibada, na namna ujumbe wa uislamu ulivyo kusanya watu wote, na ukamilifu wa dini ya kiisilamu na upole wake, na vile ilivyo mupa mwanamke haki zake.

Na utambulisho mfupi wa Nabii wa huruma Muhammad rehma na Amani iwe juu yake.

**Na tunazinduwa**

**Kama ilivyo, hakuna katazo kwa yule anaye taka kukifanyia kitabu hiki tarjama (kuigeuza katika lugha nyingine) na kukichapisha na kukizagaza, tukimuomba Allah awaongezee wote ujira na thawabu nyingi.**

**Na Allah awe ni mwenye kuteremsha rehma na amani kwa Mtume wetu Muhammad na kwa watu na wanyumbani mwake na maswahaba zake.**

## Programu ya siku ya kwanza

**10 dakika** za maandalizi

Kuwatenganisha wanawake na wanaume na kuwafahamisha walio silimu muda wa masomo na wakati utakao chukuwa kila somo na idadi ya siku za masomo.



**25 Dakika** kwa ajili ya kumpongeza muisilamu

**30 Dakika** kwa ajili ya Aqidah

**25 Dakika** za kumtambulisha kwa ufupi Nabii wa dini ya kiislamu

**Ukumbusho**

**Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.**

## SIKU YA KWANZA

### (PONGEZI KWA MUINGIYA DINI MPYA)

**Ndugu yangu muisilamu mpendwa ewe ambaye Allah amekutukuza kwa kukuongoza kwenye dini ya kiislamu hivi sasa.**

Tunakupongeza kwa kuongozwa kwako na Allah, ni yeye ndie mwenye fadhila na shukurani zote, na nihaki kwako kufurahi ni kama vile umezaliwa upya pindi ulipo ingiya ndani ya uislamu; na kuingiya kwako ndani uislamu inapelekea kufutwa (kusamehewa) ya makosa yote ulio yatenda kabla haujakuwa muislamu, na ina-ondowa kila dhambi iliyo tokea kwako kabla haujakuwa muislamu na mabaya yako yote yamefutwa.

Na ikiwa ulikuwa miongoni mwa wale walio pewa kitabu ni kwako kupata ujira mara mbili kama ilivyo pokelewa kutoka kwa Mtume wetu Muhammad rehma na amani ziwe juu lake.

**Na tunakuusia kushikamana na mambo muhimu sana, nayo ni :**

1 Niwewe kuwa mvumilivu kutokana na yale utakayo kutana nayo kutokana na matatizo za kifamilia ao kiuchumi ao mengi-neo, na yakijitokeza hayo basi hayo ni mambo ya kawaida, kila anaye silimu huwenda anakutana na hayo ispokuwa wachache,- na hali yako inafanana na hali ya maswahaba wa Mtume, bila shaka walikutana na matatizo makubwa Zaidi, walikuwa wengi miongoni mwao  wanaadhibiwa vikali sana na wakawa ni wenye kuvumilia kwa yote hayo, na mwisho wao ukawa mwisho mzuri sana duniani na hiyo siku ya mwisho (qiyama).

2 ni kwako kumshukuru Allah kwa neema ya kuongozwa kwenye uiilamu, na yule anae mshukuru Allah anakuwa ni mwenye kutenda amri zake na kujiweka mbali na kila alicho kikataza, na iliyokuwa muhimu Zaidi katika hayo ni kushikamana na swala na hasa kuzisali pamoja na watu muskitini (jamaa) ikiwezekana hilo, na kwa kusali pamoja na wengine kuna msaada kwako na kudumu kwenye ibada hiyo, amesema aliye takasika: "**Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kusali**" Suratul baqarat 45,sala ina nafasi kubwa katika uislamu na ndio nguzo kubwa za kivitendo katika nguzo za uislamu.

3 jihimize zaidi kutafuta elimu ili uweze kumuabudu Allah kwa elimu na muono, na uisilamu unahimiza watu kujifunza katika dini amesema aliye takasika: "Sema: je, wako sawa sawa wale wanao jua na wale wasio jua?" suratu zumara 9.

na imepokelewa kutoka kwa Mtume wetu muhammad rehma na amani ziwe juu lake, kwa hakika amesema: "atakaye chukuwa njia akitafuta ndani yake elimu Allah atamuwekea wepesi kupitiya njia hiyo kuelekea peponi."

4 ni kwako kujitenga mbali na kila jambo ambalo uislamu umeweza kulikataza na kusubirisha nafsi yako kwa hilo, na itakuwa haraka sana nafsi yako kuwa ni yenye kunyenyekea na kuzowea na wala haujisikii ugumu wowote, na imani yako inakuwa ngumu na imara.

5 na katika kumshukuru Allah kwa kule kukuongoza kwenye uislamu ni wewe kujaalia moyo wako uwe ni yenye huruma na upole kwa watu wako (familia) na watu wengine kwa kuwaonesha dini ya uislamu ili Allah aweze kukuandikia ujira kwa kuongoka kwao.

Ni lazima kwako kujua : kwa hakika mola wako ni mmoja, naye ni Allah, na dini yako ni uislamu, na Nabii wako ni Muhammad rehma na amani ziwe juu lake.

**Ukiulizwa nani mola wako ?**

**Basi sema :** mola wangu ni yule aliye nileya kwa neema zake, na ameniumba kutoka kutokuwepo hadi kuwepo.

**Na ukiulizwa: kwa kitu gani umemjuwa Mola wako?**

Basi sema : nimemjua kwa alama zake na viumbe vyake.

**Na ukiulizwa ni kwa lengo gani Allah kakuumba ?**

Basi sema : ameniumba kwa ajili ya kumuabudu na kumtii na kufata amri zake na kujitenga na makatazo yake; amesema aliye takasika: **{Nami sikuwaumba majini na watu ispokuwa tu kwa ajili ya kuniabudu 56,na sitaki kwao riziki,wala sitaki wanilishe 57, hakika Allah ndiye mwenye kuruzuku, mwenye nguvu, madhubuti 58}** suratu dhariyati 56-58

**Na ukiulizwa ipi dini yake?**

Basi sema: dini yangu ni uislamu, na uislamu ni kujisalimisha kwa ajili yake Allah kwa kumpwekesha na kunyenyekea kwake kwa kumtii na kujiweka mbali na shirki na washirikina, nayo ni dini ambayo Allah amewatuma mitume nayo kwa wسatu wao. Amesema aliye takasika: **{Bila shaka dini mbele ya Allah ni uislamu tu}** suratu al Imran 19**, {Na anaye tafuta dini isiyo kuwa uislamu haitakubaliwa kwake. Naye akhera atakuwa katika wenye khasara}** suratu al Imran 85

**Na ukiulizwa nani Nabii wako?**

**Basi sema:** Muhammad bni abdillah bni abdil mutwalib bni haashim, na haashim ni katika maqurayshi na maqurayshi ni katika kinana na kinana ni katika waarabu, na waarabu ni katika kizazi cha Nabii ismail bni ibrahima, na Ibrahim ni mwenye kutokana na Nuhu, Na Nuhu ni mwenye kutokana na Adam, na Adam ni mwenye kutokana na udongo, Na ushahidi ni kauli yake Allah aliye takasika: **{hakika mfano wa Isa kwa Allah ni kama mfano wa Adam; alimuumba kwa udongo kisha akamwambia: kuwa! Basi akawa}. suratu al Imran 59**

## *Utambulisho mfupi wa Nabii wetu Muhammad*

**Swali : ni nani huyo Mtume wa Allah ambaye allah alimtuma na ujumbe wa uislamu?**

Jibu : yeye ni Muhammad bni abdillah bni abdul mutwalib al hashimiy al qurayshiy, mubora wa manabii na mitume na wamwisho wao na kiongozi wao,  rehma na Amani za Allah ziwe juu yake, amezaliwa makkah mwaka wa tembo inayo wafikiana na mwaka 571 miladiya, mama yake amina binti wahbi amefariki na hali Mtume akiwa na miaka mi sita(6), akamlea babu yake Abdul mutwalib, kiisha abdul mutwalib akafariki na hali Mtume akiwa na miaka minane(8), kisha akamlea ndugu ya baba yake Abu twalib, amemuowa khadidja binti khuwaylid  na umri wake ukiwa ni wa miaka ishirini na tano(25), na ndiye mwanamke wakwanza aliye muowa na watoto wake wote amewazaa na khadidja ispokuwa tu Ibrahim.

Allah amemtuma ili afikishe ujumbe wa uislamu na umri wake ulikuwa ni wa miaka arubaini(40), akabaki makkah miaka kumi na tatu(13) akiwalingania watu kwenye tauhid yake Allah na kumpwekesha katika ibada na waachane na shirki, kisha akahamia madina na maswahaba zake watukufu, ikawa muhajiruna (swahaba waliotokea Makkah) na answari (swahaba ambayo ni wakaaji wa Madinah) jamii kubwa uliyo julikana kwa watu wa mji wa Mtume, akakaa madina miaka kumi(10) akifikisha ujumbe wa Mola wake, ufunuo ukimteremkia na akiwafunza watu hukmu za uislamu, na alikuwa ni mwenye kujihimiza sana kuwaongoza watu na kuwaokowa kuwatowa kwenye ukafiri na kuwaelekeza kwenye ibada ya mola wao, na ilikuwa ikimsumbuwa sana kule kwenda kwao kinyume na dini yake Allah.

Amefariki na umri wake ni wa miaka sitini na tatu(63), basi alifikisha ujumbe na akatekeleza amana na akanasihi ummah na akapigana katika njia yake Allah ukweli wa kupigana, na akatuacha kwenye haki iliyo kuwa wazi, hakuna kheri yoyote ila ameelekeza ummah wake kwenye kheri hiyo na hakuna shari yoyote ila ametahadharisha ummah wake kutokana na shari hiyo, na kwa hakika Allah amelazimisha waja wake waweze kumtii Mtume Muhammad  na akajaalia uongofu katika kumtii yeye Mtume, rehma na Amani zake Allah ziwe juu yake na manabii na mitume wote.

## Mpangilio wa siku ya pili

**45 Dakika**

**za qur'an**

Utambulisho wa qur'an tukufu, suratul faa-tiha kuanzia aya ya kwanza hadi ya pili

**45 Dakika**

**kwa ajili ya Fiqhi**

ya twahara, itashikwa udhu kivitendo kwa wana-funzi wote mbele ya mwalimu.

**Ukumbusho**

**Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.**

**Jambo la kwanza : ni nini hiyo qur'an takatifu?**

Qur'an ni maneno yake Allah iliyo teremshwa kwa Mtume wake Muhammad rehma na amani ziwe juu lake, na hiyo qur'an ni muujiza wakudumu yenye kuendelea mpaka pale Allah atachukuwa ardhi na waliomo ndani yake, Allah ameiteremsha ili aweze kuabudiwa kwa kuisoma na kuzingatia yaliomo na kuyafanyia kazi, amesema Allah aliye takasika: **{hakika hii bila shaka ni qur'ani tukufu, katika kitabu kilicho hifadhiwa, asiiguse yeyote ila tu msafi}** suratul waaqi'a 77-79 na amesema tena: **{na hiki kitabu, tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie aya zake, na wapate kuikumbuka watu wenye akili}** suratul swaad 29.

**Ni ipi nafasi ya qur'ani tukufu katika uislamu?**

Qur'ani tukufu inazingatiwa ndiyo asili ya kwanza miongoni mwa asili ya sheria ya kiislamu, na hakika Allah amepanga kwa usomaji wake ujira mkubwa:

Amesema Mjumbe wa Allah rehma na amani ziwe juu lake: "atakaye soma herufi moja katika kitabu cha Allah kwa hilo anapa jema moja, na jema moja ni sawa na hilo jema mara kumi, na sisemi {alifu laam miim} ni herufi moja, lakini alifun ni herufi, na laamun ni herufi, na miimun ni herufi."

**Sifa(ubora) za qur'ani tukufu :**

Kwa hakika hiyo qur'ani imelindwa kutokana na kupotoshwa na kupotea; kwa sababu Allah ameji kalifisha kuilinda kama alivyo sema aliye takasika: **{hakika sisi ndio tulio teremsha ukumbusho (quran) huu, na hakika sisi ndio tutaya hifazhi (kuilinda)}** suratul

hajr 9

Kwa hakika hiyo qur’ani ndiyo ya mwisho ya vitabu vya mbinguni na ndicho kilicho kuwa juu ya vyote, na ni miujiza yake ndio chalenji yake, hawezi yeyote yule kuleta mfano wake hata aya moja?

wepesi na uraisi kuyahifazhi kama alivyo sema aliye takasika: **{na bila shaka sisi tumeifanya qur’ani iwe nyepesi kufahamika. Lakini yupo anaye kumbuka?}** suratul qamar 17

Jambo la pili: kuhifazhi suratul faatiha na baadhi ya sura fupi fupi; kwa sababu ya kuzisoma ndani ya swala na kumuabu Allah kwa kuisoma qur’ani, kama tunavyo lazimisha kwa kila mwanafunzi kufanya hili ni sehemu ya kuanziya kuisoma na kuhifadhi qur’ani yote nzima.

Na inapendekezwa kwa mwalimu kufunguwa moja ya programu za qur’ani inayo patikana katika djad-wali (horaire), na awasikilizishe wanafunzi kisomo cha mmoja wa wasomi wanao wapendwa, na awaombe wanafunzi waweze kumsikiliza na warejelee rejelee baada yake, na mwalimu awafatiliye na kuhakikisha kwamba matamshi yao ya qur’ani ni sahihi.

Na ni bora kuchaguwa (application ya minshawi mwalimu wa qur’ani) ambayo inarudiliya pamoja na msomaji na hii ndio njia nyepesi kwa wanafunzi kuijuwa vyema na ni sahihi Zaidi kwa kuhifadhi kwao na kuwa mbali na makosa.

Ni vyema pia kwa mwalimu kuwawekea wazi wanafunzi maana ya aya kiufupi.



سُورَةُ الفَاتِحَةِ ١

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ١
ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٢
ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ٣ مَٰلِكِ يَوۡمِ ٱلدِّينِ ٤
إِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَإِيَّاكَ نَسۡتَعِينُ ٥ ٱهۡدِنَا
ٱلصِّرَٰطَ ٱلۡمُسۡتَقِيمَ ٦ صِرَٰطَ ٱلَّذِينَ أَنۡعَمۡتَ
عَلَيۡهِمۡ غَيۡرِ ٱلۡمَغۡضُوبِ عَلَيۡهِمۡ
وَلَا ٱلضَّآلِّينَ ٧

وَآيَاتُهَا سَبۡعٌ

## Fiqhi

### Ni nini fiqhi?

Maana yake kilugha: kuelewa(kufahamu), Maana ya fiqhi kisheria: ni kujua hukmu za kisheria kwa ushahidi wake, nazo ni aya za qur'ani na hadithi za Mtume rehma na amani ziwe juu lake.

### Ni fadhila gani anazo zipata anae jifunza katika dini?

Amesema Mtume wa Allah rehma na amani zimfikie: "yule ambae Allah humtakia kheri (duniani na akhera), basi humpa ufahamu katika dini". Kaipokea hadith hii imam bukhari

Na Hapa tunakuwekea mukhtasari wa mambo muhimu ambayo ni lazima uyajue kutokana na hukumu za dini yako:

## *Jambo la kwanza : twahara(kujisafisha) na hukumu zake:*

1. utambulisho wa neno twahara:

Nayo ni kuondowa hadathi(uchafu) kwa kutawadha ao kuoga ao kutayammam, na kuondowa najisi kwenye mwili, mavazi na kwenye ardhi.

Najisi inaondoshwa kwa kitu gani?

najisi inayo toka kwenye njia mbili (haja kubwa na ndogo) Inaondoshwa kwa maji ao jiwe ao kwa mouchoirs na mfano wake, na ima kinyume na yale yanayo toka katika njia mbili (haja ndogo ao kubwa) mfano nguo na ardhi basi najisi inaondoka kwa kuondoka kwa athari yake ima inaweza ikawa kwa maji ao kitu kingine hata kwa jua na kwa hewa.

2. Namna ya kushika udhu : unaosha vitanga vyako viwili vya mikono, kisha unaweka maji kinywani na kupandisha maji puwani (nikuvuta maji yaingiye ndani ya pua kisha unayaondowa) na un-

aosha uso wako (kipimo cha uso ni: kuanzia sehemu ya maoteo ya nyele hadi kwenye ndevu kwa kwa urefu, na kuanzia kwenye sikiyo hadi sikiyo nyingine kwa upana), kisha unaosha mkono wako wakulia kuanzia kwenye ncha ya vidole hadi kwenye fundo ya maunganiyo kisha mkono wako wa kushoto unafanya mfano wa hivo, kisha unapaga maji ku kichwa chako kizima pamoja na masikio mara moja, kisha unaosha mguu wako wakulia hadi kwenye fundo mbili za miguu kisha mguu wa kushoto unafanya mfano wa hivo, na udhu huu unaitwa udhu wakutosheleza. Na ima udhu kamili nayo nikuosha kila kiungo mara mbili ao mara tatu, ispokuwa kichwa na masikio zinapagwa mara moja.

Na ni sunna kusema: (Bismillah) kabla ya kuanza kushika udhu. Kama ilivyo kuwa sunna kuomba dua hii baada ya kushika udhu: **"ASH-HADU ANLAA ILAAHA ILALLAAHU WAHDAHU LAA SHARIIKA LAHU, WA ASH-HADU ANNA MUHAMMADAN ABDUHU WA RASUULUHU", "ALLAHUMMA JE'AL-NII MINATAWAABIINA WA JE'ALNII MINAL MUTATWAHIRIINA".**

3 vitenguzi vya udhu : ni kila kinacho toka kwenye njia mbili (haja kubwa na ndogo, pumzi, majii ya uzazi(manii), maji ya matamanivu (madhii) na wadii na damu) na usingizi unao poteza ufahamu, na kutenda tendo la ndoa (kujaamiana).

4 Namna ya kuoga josho kubwa, nayo ina namna mbili:

Namna ya kwanza: kuoga unao tosheleza, nao ni mtu kumuagia maji kwenye mwili wote mzima.

Namna ya pili : kuoga kwa ukamilifu na namna yake: nikushika uzhu kisha mtu ana mwagilia maji kichwani mara tatu, kisha anaosha upande wa kulia wa mwili, kisha anaosha upande wa kushoto, kisha anaosha mwili mzima(kueneza maji mwili mzima).

5 Ni lazima mtu aoge josho kubwa kutokana na moja mwa hali tatu :

Wakati inapotoka maji ya uzazi (manii) ima inaweza ikawa mtu yuko macho ao wakati wakujilotea wakati amelala.

Kwa kutenda tendo la ndoa hata kama maji ya uzazi (manii) hayakutoka.

Wakati mwanamke anapo safika kutoka katika ada yake ya kila mwezi (hedhi) ao baada ya kukauka kwa damu ya uzazi (ni-fasi).

Na inapendeza (sunna) kuoga siku ya ijuma kabla ya kuenda muskitini, na siku ya idi mbili, na wakati mtu anapoingiya ndani ya uislamu.

### 6. Tayammam : ni wakati gani ni sheria mtu kutayammam ?

Imewekwa sheria kwa mtu ambaye hakuweza kupata maji, au asiye weza kutumia maji kwa sababu ya ugonjwa au sababu nyingine. Na nisunna kusema "BISMILLAH" wakati wa kutayammam.

Na namna ya kutayammam: ni kupiga vitanga viwili vya miko-no kwenye ardhi kisha unapaga uso kwa vitanga hivyo na nje ya vitanga (nyuma ya vitanga).

### 7. Na ni zipi sunna za kimaumbile ?

Nazo : 1)Al Istihdad : nayo nikunyowa nyele za sehemu ya siri.

2) Al khitani (kutaili ao kukata jando): nayo nikukata ngozi iliyo zidi ambayo inayo funika kichwa cha tupu ya mwanaume baada ya kuzaliwa, ima yule aliye silimu na ni mkubwa akiweza kutailiwa bila ya mazhara basi akate ngozi hiyo, ima ikiwa itam-leteya mazhara basi asiyafanye (asiyakate).

3) kupunguza masharubu : nayo ni zile nyele zinazo ota juu ya mdomo wajuu.

4) kungoa nyele za kwapa : nayo nikuondowa nyele zinazo kuwa kwapani.

5) kukata kucha.

## Programu ya siku ya tatu

**45 Dakika** – kwa ajili ya qur'ani

- suratul faatiha kuanzia aya ya 3 hadi ya 4

**45 Dakika** – kwa ajili ya fiqhi

- sala na sharti zake

### Ukumbusho

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.


سُورَةُ ٱلْفَاتِحَةِ ١

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ١
ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٢
ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ٣ مَٰلِكِ يَوۡمِ ٱلدِّينِ ٤
إِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَإِيَّاكَ نَسۡتَعِينُ ٥ ٱهۡدِنَا
ٱلصِّرَٰطَ ٱلۡمُسۡتَقِيمَ ٦ صِرَٰطَ ٱلَّذِينَ أَنۡعَمۡتَ
عَلَيۡهِمۡ غَيۡرِ ٱلۡمَغۡضُوبِ عَلَيۡهِمۡ
وَلَا ٱلضَّآلِّينَ ٧

وَآيَاتُهَا سَبْعٌ

## *Jambo la pili : sala na baazhi za hukumu zake :*

### Kipengele cha kwanza : nafasi ya swala katika dini ya uislamu:

Swala ina sehemu kubwa kwenye uislamu ; nayo ni ibada pekee ambayo iliyo faradhishwa mbinguni wakati Mtume (rehma na amani zimfikie) alipo pandishwa mbinguni, na ni nguzo ya pili katika nguzo za uislamu, na ndiyo nguzo kubwa ya uislam na ndiyo tofauti iliyoko kati ya muislamu na kafiri, na ambaye atakaye iacha bila shaka amekufuru, na ndiyo itakuwa jambo la kwanza ambayo mja ataulizwa hiyo siku ya kiyama katika matendo yake, basi swala yake ikikubaliwa matendo yake mengine yatakubaliwa, na ikirejeshwa basi matendo yake mengine yatarejeshwa, atakaye isimamisha swala hiyo itamuzuwiya na mambo machafu na maovu na madhambi, na kupitia swala mtu hujisaidia kwa kutatua matatizo ya maisha na mazito inayo mfikiya mtu, swala hufuta madhambi na makosa, na mja ni mwenye kuhitaji saana yale ambayo yatamfutiya (kumzimiya) madhambi yake anayo yakosea kwa ku kusidiya ao kwa kuto kukusudiya, basi swala itakuja kuiweka mizani yake ya mema kuwa mzito na itamuweka mbali na moto wa jahanama na itamsogeza Zaidi kuwa karibu na pepo.

Na yule anaye taka kutizama nafasi ya uislamu moyoni mwake, basi ni yeye kuweza kutizama nafasi ya swala nafsini mwake, ikiwa ni mwenye kuiheshimu swala na kuipenda na akawa ni mwenye kuipupia, basi hii ni ushahidi tosha wa Imani yake na mapenzi yake ya hii dini.

Na swala haianguki (yaani mtu kuiacha swala) kwa muislamu kwa hali yoyote ile maadamu akili yake ingaliki, basi asali kutokana na hali yake, swala haianguki (yaani haachi kusali) kwa mugon-

jwa na aisali swala hiyo kwa hali yoyote ile awe amesimama ao ameikaa ao amelala ubavu ao amelalia mugongo: awe na ashiria kwa kichwa chake akiwa ni mwenye kuenda rukuu na sijida, na swala haianguki wakati wa woga na mapambano, na lau ikikadiriwa kwa hakika amekosa maji na udongo, mfano mfungwa na mugonjwa ambaye hawezi na hana yeyote yule wakumsaidia kushika udhu, na hana yeyote yule wakumletea udongo, kwa hakika ni yeye asali na wala asiachi swala na wala asi isali swala hiyo nje ya wakati wake hata kama atakuwa hakukamilisha baadhi ya sharti zake na hata lau akisali bila ya udhu wala tayammam.

**Jambo la pili : Nyakati za swala :**

Kusali swala kwa wakati wake ni jambo ya lazima, kwa kauli yake Allah :

**{Kwani hakika swala kwa waumini ni faradhi iliyo wekewa nyakati maalumu }** suratu nisai : 103. : kwa maana iliyo faradhishwa.

Na ni haramu kuicheleweshа kwa kuitowa nje ya wakati wake; na kuitowa nje ya wakati wake kwa kusudi inapelekea mtu kuto kukubaliwa swala yake, na kitendo hicho nikatika madhambi makubwa. Na kwa hiyo, mtu ni wajibu kwake kuitekeleza kwa wakati wake na hata akiwa hawezi kushika udhu ao hajuwi kibla ni wapi ao akawa ni msafiri hangani ao baharini ao vinginevyo ni lazima kwake kuisali kwa wakati wake sawa na uwezo wake na hali yake.

## *Kubainisha nyakati za Swalah tano za farazhi:*

| Idadi | Wakati | Swala | Rakaa |
| --- | --- | --- | --- |
| 2 | Kuanzia alfajiri ya ukweli kucho-moza hadi jua kuchomoza | Al fajiri | Rakaa 2 |
| 4 | Itakapo mili jua kuelekea magharibi mpaka pale kuvuli cha kila kitu kitakuwa sawa na mfano wake | Adhuhuri | Rakaa 4 |
| 4 | Kuanzia mwisho wa sala ya adhuhuri mpaka pale jua ita-chukuwa rangi ya njano(jaune) | Asri | Rakaa 4 |
| 3 | Ni baada ya kuzama kwa jua hadi itakapo zama mawingu mekun-du | Maghrib | Rakaa 3 |
| 4 | Baada ya kuzama kwa mawingu mi-kundi hadi kati kati ya usiku | Ishai | Rakaa 4 |

## *Jambo la tatu : sharti za swala ni tisa, nazo ni :*

Uislamu, akili, kupambanukiwa, kustiri uchi, kuondowa hadith(kubwa ao ndogo, yaani kushika udhu ao kuoga), kuondowa najisi, kuelekea kibla, kuingiya kwa wakati wa swala, na kuweka nia.

## Programu ya siku ya nne

**45 Dakika** ya qur 'ani

Kusoma suratul Faatiha kuanzia aya ya 5 hadi ya sita.

**45 Dakika** ya Fiqhi

Namna ya kusali: itatekelezwa namna ya kusali kwa vitendo kwa wanafunzi wote mbele ya mwalimu

**Ukumbusho**

The lesson should be repeated on a daily basis at three intervals in order to take into account the times of all the followers. Some of them are suitable for the morning, some for the afternoon and some for the evening, and for anyone who would like to be attendance again to get more understanding.


سُورَةُ الفَاتِحَةِ ١
بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ١
ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٢
ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ٣ مَٰلِكِ يَوۡمِ ٱلدِّينِ ٤
إِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَإِيَّاكَ نَسۡتَعِينُ ٥ ٱهۡدِنَا
ٱلصِّرَٰطَ ٱلۡمُسۡتَقِيمَ ٦ صِرَٰطَ ٱلَّذِينَ أَنۡعَمۡتَ
عَلَيۡهِمۡ غَيۡرِ ٱلۡمَغۡضُوبِ عَلَيۡهِمۡ
وَلَا ٱلضَّآلِّينَ ٧
وَآيَاتُهَا سَبۡعٌ

## *Jambo la nne : namna ya kusali :*

Unaelekea kibla kisha unasema : " ALLAHU AKBAR"(takbiratul ihramu) na unasoma suratul faatiha na unasoma chochote kilicho kuwa chepesi katika qur'ani, kisha unaenda rukuu ukisema: "ALLAHU AKBAR" na unasema ukiwa kwenye rukuu: **"SUBHANA RABIYAL ADHWIIM"** mara moja na ukizidisha ni bora Zaidi, kisha unatoka kwenye rukuu ukisema: **"SAMI'ALLAHU LIMAN HAMIDAH", "RABANA WALAKAL HAMDU",** ukiwa wewe ni maamuma inatosha kwako kusema tu: **"RABANA WALAKAL HAMDU"** bila kusema **"SAMI'ALLAHU LIMAN HAMIDAH",** kisha unasema "ALLAHU AKBAR" kwa kuelekea sijda, kisha unasema ukiwa sijda: **"SUBHANA RABIYAL A'ALAA"** mara moja na ukizidisha ni bora Zaidi.

Kisha unainuwa kichwa chako kutokea sijida ukisema: "ALLAHU AKBAR", kisha unaikaa na unasema unapo kuwa umeikaa: **"RABBIGH FIIRLI**" mara moja na ukizidisha ni bora Zaidi, kisha unasujudu mara ya pili ukisema:" ALLAHU AKBAR", na unasema ukiwa sijda: **"SUBHANA RABIYAL A'ALAA**", mara moja ukizidisha ni bora Zaidi, kisha unainuka kutoka sijda ya pili ukisema: "ALLAHU AKBAR" kuelekea kwenye rakaa ya pili, kisha utafanya kwenye rakaa ya pili kama ulivyo fanya kwenye rakaa ya kwanza.

Na utakapo maliza sijda ya pili kwenye rakaa ya pili utaikaa na unasoma: **"ATTAHIYATU LILAHI WAS SWALAWATU WATWAYYIBATU, ASSALAMU 'ALAYKA AYUHAN NABIYYU WARAHMATULLAHI WABARAKATUHU, ASSALAMU 'ALAYNA WA 'ALA 'IBADILAHI SWALIHINA, ASH HADU ANLA ILAHA ILALLAHU WA**

**ASH HADU ANNA MUHAMMADAN ’ABDUHU WA RASULUHU,** kisha unasema: **ALLAHUMA SWALLI ’ALA MUHAMMADIN WA ’ALA ALI MUHAMMADIN KAMAA SWALAYTA ’ALA IBRAHIMA WA ’ALA ALI IBRAHIMA INNAKA HAMIDUN MAJIID, WA BAARIK ’ALA MUHAMMADIN WA ’ALA ALI MUHAMMADIN KAMA BAARAKTA ’ALA IBRAHIMA WA ’ALA ALI IBRAHIMA INNAKA HAMIDUN MAJIID”** na nisunna kusema baada ya kosoma hayo **“AU’ZHU BILAHI MIN ’AZHABI JAHANNAMA WAMIN ’AZHABIL QABRI WA MIN FITNATIL MAHYAA WAL MAAMATI WAMIN FITNATIL MASIIHI DAJAL”.**

Kisha unatowa salamu ukigeuka upande wakuume ukisema: **“ASSALAMU ’ALAYKUM WA RAHMATULLAHI”**,kisha unageuka upande wa kushoto ukisema: **“ASSALAMU ’ALAYKUM WARAHMATULLAHI”**

**Na kwa hayo yote sala ya rakaa mbili itakuwa ime malizika.**

Na ikiwa ni swala ya rakaa tatu ao rakaa nne, utakapo maliza sijda ya pili kwenye rakaa ya pili utaikaa na unasoma: **“ATTAHIYATU LILAHI... mpaka mwisho wa tashahudu**”, kisha unasimama ukisema:” ALLAHU AKBAR” kisha utasali rakaa zingine zilizo baki mfano wa vile ulivyo Sali rakaa ya kwanza na utatosheka kusoma suratul faatiha na hauto soma chochcote baada yake, Baada ya rakaa ya mwisho ya sala ya rakaa tatu au nne, utakapo maliza kusujudu, utakaa tashahhud ya mwisho ukisoma:

Atahiyyatu lilahi yote mzima, na kumsalia Mtume, na kujikinga na sheytwan, na kutowa salamu kama ulivyo fanya ulipo towa salamu kwenye sala ya rakaa mbili.

Zinduo : haijuzu kuinuwa macho juu mbinguni wakati wa sala, kwa sababu ni katika mambo ya haramu ndani ya sala.

### Ni nini anayo yasema muislamu mpya ndani ya swala yake?

Ufupi wa yale anayoyasema Muislamu mpya katika swala yake, ni kwa mujibu wa hadith iliyo elekeza kutoka kwa Mtume sala na salamu zimuendee:

**Baada ya takbiratul ihram wakati unapo simama:**

Ikiwa mtu haifazhi suratul faatiha atasoma yale yatakayo kuwa mepesi kwake katika qur'ani; akiwa na uwezo asome aya saba, na asipo kuwa na uwezo huo aseme: **"SUBHANALLAHI WAL HAMDULILAHI WA LA ILAHA ILALLAHU WALLAHU AKBAR WALA HAULA WALA QUWATA ILA BILAHI"**, na asipo wezeshwa kuleta dua zinazo somwa kwenye rukuu na sijida basi aseme: **"SUBHANALLAH"** na hivo hivo akitoka rukuu amuhimidi Allah **(ALHAMDULILLAH)** na aombe kati ya sijida mbili. Na atakapo kuwa kwenye tashahhud na akawa si mwenye kuhifadhi dua ya tashahud, nikwake kumuhimidi Allah (Alhamdulillah) na kumsabihi (subhanallah) na kumukabir (Allahu akbar) na kumsalia Mtume na aombe dua yake. Kiasi kwamba hapakupokelewa chochote kuhusu hayo tuliyo yaashiria.

Na kila tulicho kitaja nikwake akilete kwa kadiri ya uwezo wake, na asipo weza kusema chochote katika nyiradi za ndani ya swala, ila huku katekeleza nguzo zote za swala za kivitendo basi swala yake ni sahihi, kwa sababu iwe nguzo gani ya swala ao sharti ao jambo ya lazima ndani ya swala ni yenye kuanguka endapo mtu hatokuwa na uwezo wakuitekeleza. Kwa hiyo, kuwafundisha ni ya lazima kuwa upole na taratibu (hatua kwa hatua).

Na hii haimaanishi mtu awe mzembe katika utafutaji wa elimu iliyo kuwa ya lazima kwake kuijuwa. Ni lazima ajitolee kwa kadri ya uwezo wake, kama kuhifazhi suratul faatiha na yale yatakayo kuwa mepesi kwake katika qur'ani na hivo hivo yale yanayo somwa kwenye nguzo zote za swalah na tashahhud

**Na ni sunna kusoma nyiradi hizi baada ya kutowa salamu ya swala ya faradhi:**

Astaghfirullah, astaghfirullah, astaghfirullah. Allahumma anta salamu waminka salamu tabaarakta ya zhal jalali wal ikraam. Laa ilaha ilallahu wahdahu laa sharikalahu, lahul mulku walahul hamdu wa huwa ’ala kulli shay-in qadiir, Allahumma laa maania’ lima a’atwayta walaa mu’utwiya lima mana’ata, wala yanfau’ zhal jaddi minkal jadd.

La ilaha ilallahu wahdahu la shariikalahu, lahul mulku, walahul hamdu, wa huwa ‘ala kulli shay-in qadiir, la haulaa wala quwata ila bilahi, la ilaha ilallahu, wala na’abudu ila iyyahu, lahul ni’imatu walahul fadlu walahu thanaaul husana, laa ilaha ilallahu mukhliswiina lahu dina walau karihal kaafiruun.

**Kisha unasema:** Subhanallah mara 33, walhamdulillah mara 33, wallahu akbar mara 33, itakuwa jumla yake mara 99. Kisha utakamilisha 100 kwa kusema: La ilaha ilallahu wahdahu la shariikalahu, lahul mulku, walahul hamdu, wa huwa ‘ala kulli shay-in qadiir. Atakaye sema hayo atasamehewa madhambi yake hata zikiwa mfano wa povu la bahari.

**Kisha anasoma Ayatul kursiyyi,** nayo ni kauli yake Allah: **{ALLAHU LAA ILAHA ILA HUWAL HAYYUL QAYYUM, LAA TAAKHUDHUHU SINATUN WALA NAUM, LAHU MAA FI SAMAAWAATI WAMA FIL ARDWI, MAN DHAL LADHI YASHFAU’ I’INDAHU ILA BI IDHNIHI, YA’LAMU MAA BAYNA AYDIIHIM WAMA KHALFAHAM, WALAA YUHITWUNA BISHAYIN MIN I’LMIHI ILA BIMA SHAA, WASIA’ KURSIYUHU SAMAWATI WAL ARDWI, WALAA YA UDUHU HIFDHUHUMA WAHUWAL A’LIYUL A’DHWIM}** suratul baqara 255

**Kisha unasoma sura tofauti:** Qul au’dhu birabil falaq, qul au’dhu birabin naasi.

## Programu ya siku ya nne

**45 Dakika** — za qur'ani

- Suratul faatiha aya ya 7

**45 Dakika** — fiqhi

- Swala kipengele cha(5,6,7,8)

**Ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

سُورَةُ الفَاتِحَةِ ١

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ١
ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٢
ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ٣ مَٰلِكِ يَوۡمِ ٱلدِّينِ ٤
إِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَإِيَّاكَ نَسۡتَعِينُ ٥ ٱهۡدِنَا
ٱلصِّرَٰطَ ٱلۡمُسۡتَقِيمَ ٦ صِرَٰطَ ٱلَّذِينَ أَنۡعَمۡتَ
عَلَيۡهِمۡ غَيۡرِ ٱلۡمَغۡضُوبِ عَلَيۡهِمۡ
وَلَا ٱلضَّآلِّينَ ٧

وَآيَاتُهَا سَبۡعٌ

### *Jambo la tano : inayo chukizwa ndani ya swalah :*

Kugeuka geuka bila yakuwa na shida na hilo, kutizama yale yanayo mupumbaza na kumtowa nje ya swalah, nakufungia mikono miwili kiunoni na kutandaza mikono yake chini wakati wakusujudu.

### *Jambo la sita : yanayo haribu swalah :*

Ni kila kinacho haribu udhu, na kuipa kibla mugongo, na kuongeza nguzo za sala na kuzipunguza kwa kusudi, na kuharibu nia ya swalah, na kula na kunywa, na kuzungumza maneno ya nje ya swalah, na kufichua sehemu za siri kwa kusudi (na sehemu za siri za mwanaume ni kuanzia kwenye kitofu mpaka kwenye magoti, na ima mwanamke mwili wake wote mzima ni utupu ispokuwa uso ndani ya swalah sio tupu ikiwa pembezoni mwake hakuna mwanaume mgeni(ajnabiy)).

### *Jambo la saba : kuna zingine sala muhimu sana katika uislamu :*

Swala ya ijuma : nayo ni swalah ya faradhi kwa kila muisilamu mwanaume siku ya ijuma(vendredi), badala ya sala ya adhuhuri.

Sala mbili za Idi asubuhi ya siku ya idi : nayo ni faradhi ya kutosheleza kwa wanaume,  nani sunna kwa wanawake.

Na ni sunna siku ya ijuma na idi mbili kuoga na kujisafisha na kuvaa mavazi mazuri na kujipulizia mafuta uzuri(parfum)na mengineo

Swala ya kupatwa kwa jua ao mwezi:  ni sunna kuisali, inasaliwa pindi jua inapo patwa ao mwezi unapo patwa.

Swala ya kuomba nvua : ni sunna, husaliwa pindi nvua inapoku-

wa ndogo na maji, na ardhi ikawa kavu, yaani ikawa haina mimea.

Swala ya jeneza: nayo ni faradhi ya kutosheleza. Na maana ya faradhi ya kutosheleza: ni jambo lililo kuwa la lazima kutekelezwa kwa baadhi ya waisilamu, na wasipo litekeleza kwa hakika wote wanakuwa ni wenye kupata dhambi.

## Jambo la nane : Swalah za sunna :

**Umuhimu wake :** Swala ya sunna ina umuhimu mkubwa katika Uislamu, kwa sababu sala hizo zinakamilisha upungufu ulio patikana katika sala za faradhi, Kumleta mja karibu na mapenzi ya Allah kwake, Na pindi Allah anapo mpenda mja wake, humwongoza katika kila jema na humuepusha na kila shari.

Na katika aina zake :

**Swalah ya witri :** nayo ni rakaa moja ao tatu ao tano ao saba ao tisa ao kumi na moja,haina kiwango maalumu kutokana na uwingi wake, kwa hivyo anaswali usiku awezavyo, kisha anamaliza Swalah yake kwa rakaa moja, na wakati wa swalah ya witri ni baada ya sala ya lishai mpaka wakati wa sala ya alfajiri, na kuisali wakati wakuelekea mwisho wa usiku ndio bora Zaidi.

Swalah za sunna zinazo saliwa kabla na baada ya sala ya faradhi: idadi yake ni rakaa kumi na mbili: rakaa mbili kabla ya alfajiri, na rakaa nne kabla ya adhuhuri na rakaa mbili baada yake, na rakaa mbili baada ya maghrib, na rakaa mbili baada ya lishai. Na ubora wa sunna hizi ni kubwa mno: Amesema Mtume sala na salamu zimfikiye: “Hawi mja Muislamu yeyote yule anaye sali kwa ajili ya Allah kwa kila siku rakaa kumi na mbili za sunna zisizokuwa faradhi, ila Allah atamjengea nyumba peponi”. Kaipokea imam muslim

Swalah ya dwuha : uchache wa rakaa zake ni mbili na uwingi wake ni rakaa nane, na wakati wake wakusaliwa ni baada ya

jua kuchomoza kwa robo saa(dakika 15) mpaka kabla ya kuingiya kwa swalah ya adhuhuri kwa robo saa.

Swalah za sunna zilizo achiwa yaani zisizo kuwa na sababu: nayo ni mtu kusali rakaa anazo zitaka bila ya idadi maalumu kwa sababu Allah anapendaga swalah, lakini usisali swalah zasunna katika nyakati zilizo katazwa kusali ndanimo, nayo ni nyakati tatu:

**Ya kwanza:** ni baada ya swalah ya alfajiri mpaka baada ya jua kuchomoza kwa robo saa.

**Ya pili :** kabla ya kuingiya kwa swalah ya adhuhuri kwa robo saa, wakati huo unaitwa wakati wakumili kwa jua kuelekea magharibi.

**Ya tatu :** ni baada ya swalah ya laasir hadi wakati wa jua kuzama.

## Programu ya siku ya sita

**45 minutes** za qur'ani

Suratul faatiha( wanafunzi wote kuihifadhi), na kuleta tafsiri ya suratul faatiha kiufupi.

**45 Dakika** za Fiqhi

Twahara(kujisafisha) na swalah(utelekezaji waswalah kivitendo kwa wanafunzi wote)

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

## *Tafsiri fupi(mukhtasari ) ya Suratul Faatihah*

**Kauli yake Allah :** {bismillah} : kwa maana ninaanza kauli yangu kama kusoma ao kitendo changu kama kuandika: kwa jina la Allah; ili shetani awe mbali na Baraka za Allah(ar'rahmani) ziteremke, na nikiitaji msaada wake katika hauli yangu na kitendo change

**{Allah}:** ni neno la aliye tukuka, nayo ni jina la Mwenyezi Mungu, na wala halitumiwi kwa yeyote yule kinyume yake yeye, na maana yake: Muabudiwa anaye stahiki kuabudiwa yeye mwenyewe bila ya kushirikishwa na yeyote yule, kwa kusifika kwake kwa sifa za utukufu na ukamilifu, Utukufu ni Wake yeye Allah.

{Mwingi wa rehema mwenye kurehemu}: ni jina mbili zinazo onesha ya kwamba yeye Allah ni mwenye rehema kubwa tena pana ambayo imekusanya viumbe vyote, na Allah ame wahusisha waumini kwa rehema yake iliyo kamilika.

**Kauli yake :** {sifa njema zote niza Mwenyezi Mungu, mola mlezi wa viumbe vyote}**:** Alhamdu ni sifa njema kwa ukamilifu isiyokuwa na mpaka kwa kila hali.

{Mola mlezi wa viumbe vyote} : **Mola Mlezi**: Yeye ndiye mlezi wa walimwengu kwa kuwaumba na kusimamia mambo yao, Na walimwengu: wote ni viumbe, kila kitu kisicho kuwa Mwenyezi Mungu ni ulimwengu(kiumbe).

**Kauli yake Allah :** {Mwingi warehema mwenye kurehemu} : maana yake imetangulia kwenye maana ya neno bismillah.

**Kauli yake Allah :** { Mwenye kimiliki siku ya malipo}: siku ya malipo ni siku ya mwisho(kiyama).

**Na mwenye kumiliki ni:** msimamizi(mwendeshaji) wa kila

kitu, anayo amri(kuamrisha) na katazo(kukataza), msamaha, adhabu, na kadhalika, na yeye ndiye mumiliki wa dunia na akhera, lakini amehusisha siku ya kiama kwa ufalme; kwa kuonekana kwake kiukamilifu kwa viumbe vyake, na kujisalimisha kwa wafalme wote wa dunia ambao walijidai ubwana na ufalme katika ulimwengu bila haki, kama vile Firauni na wengine.

**Kauli yake Allah : {**Wewe tu tunakuabudu, na wewe tu tunakuomba msaada**}** :yaani tunakuhusisha peke yako katika ibada na kukuomba msaada, hatuabudu ila wewe na hatutaki msaada ia kwako.

Alitaja kutaka msaada baada ya ibada pamoja na kwamba kutaka msaada ni sehemu ya ibada kwa kule mja katika ibada zake zote anahitaji kumtaka Allah msaada na lau Allah asingemsaidia asingepata anachotaka katika kufanya maamrisho na kujiweka mbali na makatazo, kwa hiyo inapendeza kumuomba Allah daima na hasa kwenye tashahudi ya mwisho unapo Sali, unasema: “Ewe Mola wangu nisaidiye kwenye jambo lakukutaja Zaidi na kukushukuru na kuifanya ibada yako iwe nzuri”.

**Na Ibada ni** : kila anacho kipenda Allah na kukiridhia katika maneno na vitendo vya wazi na vya siri.

**Na kutaka msaada ni:** Kumtegemea Allah kwa kutaka kufikiwa na mambo mazuri na kuepushiwa na mambo mabaya, huku ukiwa na matumaini kwake kwa kufikiwa na hilo.

**Kauli yake Allah :{** Tuongoe njia iliyo nyooka**}** :yaani Tuongoze kwenye njia iliyonyooka, na utujaalie kuifanikisha.

Kwa hivyo ombi la Muislamu la kutaka uongofu lina maana ya kuomba kuzidishiwa katika uongofu huo, na kuthibiti ndani yake na kufa juu yake, na njia iliyonyooka ni njia ya wale ambao Allah amewabariki katika mitume,na wakweli, na mashahidi na watu wema.

**Kauli yake Allah : {**siyo ya walio kasirikiwa, wala walio potea**}** yaani sio njia{ siyo ya walio kasirikiwa}: na hao ndio walio tambuwa haki wakaiacha, ao wameigeuza na kuibadili kama mayahudi, { na wala}: si njia ya {walio potea} :ambao walio muabadu Allah kwa ujinga na waliiacha haki kwa ujinga na upotofu kama Wakristo(wanaswara).

**Na neno:** amiin, si katika suratul faatiha, na maana yake : Ewe mola jibu, na inapendeza kusema amiin baada kusoma suratul faatiha ikiwa ndani ya swala ao nje ya swala.

## Programu ya siku ya saba

**Saa moja na nusu kwa ajili**

- ya qur'an



- Itakuwa kufundisha suratul ikhlas yote kamili, tafsiri fupi(mukhtasar) ya suratul ikhlas

**Ukumbusho**



Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

# سُورَةُ الإِخْلَاصِ

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ﴿٢﴾ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ﴿٣﴾
وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدٌۢ ﴿٤﴾

## *Tafsiri fupi(mukhtasar) ya suratul ikhlas*

Kwa jina la Mwemyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu.

{Sema : yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee1, Mwenyezi Mungu mkusudiwa2, hakuzaa wala kuzaliwa3, wala hana anaye fanana naye hata mmoja4}

Yaani : {Sema}kauli iliyokuwa thabiti, ukiiamini, na mwenye kujua maana yake.

{yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee}: Yaani Umoja umefungiwa Kwake, Yeye ndiye mmoja aliye jipwekesha kwa ukamilifu, ambaye anayo Majina Mazuri Zaidi, na Sifa Zilizo Juu Kamilifu, na Matendo Matakatifu, asiye na mfano wake.

{ Mwenyezi Mungu mkusudiwa }: yaani anaye kusudiwa kwenye shida zote, walio kuwa juu mbinguni na walioko ardhini wote ni wenye kumuhitaji yeye Allah ukweli wakumuitaji, wanamuomba kutokana na shida zao, Na wanamtaka katika kazi zao, kwa sababu amekamilika katika sifa zake, mjuzi aliye kamilika ka-

tika elimu yake, mpole aliye kamilika katika upole wake, mwenye huruma aliye kamilika katika huruma wake ambao umeenea kila kitu, na hivo hivo sifa zake zingine, na katika ukamilifu wake nikwamba:

{ hakuzaa wala kuzaliwa } : kwa ukamilifu wa utajiri wake.

{wala hana anaye fanana naye hata mmoja}: sikatika jina zake wala katika sifa zake wala katika matendo yake, ametakasika aliye juu.

**Sura hii imekusanyika kwenye kumpwekesha Allah.**

## Programu ya siku ya Nane

**45 Dakika** za qur'ani

Kuhifadhi suratul ikhlas yote kamili kwa wanafunzi wote

**45 Dakika** za Aqidah(itikadi)

mipangilio ya dini na nguzo za uislamu

**Ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

## سُورَةُ الإخلاص

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلۡ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ١ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ٢ لَمۡ يَلِدۡ وَلَمۡ يُولَدۡ ٣
وَلَمۡ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدُۢ ٤

Zinduo

**Ni lazima mwanafunzi kuhifadhi nguzo za uislamu na imani.**

**Utakapo ulizwa ni ipi mipangilio ya dini ambayo imejenga dini juu yake?**

Basi sema mipangilio ya dini ni tatu nazo ni :

1. Uislamu 2. Imani 3. Ihsani(wema)

**Na kwa ufafanuzi zaidi ni kama ifatavyo:**

## Mpangilio wa kwanza : Uisilamu

**Uislamu ina nguzo tano :** nayo ni kushuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allah na Muhammad ni Mtume wa Allah, na kusimamisha swala, na kutowa zaka, na kufunga mwezi wa ramadhani, na kukusudia(kuhiji) nyumba tukufu ya Makkah kwa mwenye kuwa na uwezo ya kuendea.

Nguzo ya kwanza : Kushuhudia ya kwamba hakuna apasae kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allah na kwa hakika Muhammad ni Mtume wake:

Na shahada hii ndiyo ufunguo wa uislamu na msingi wake ambawo imejengeka juu yake.

**Na nini maana ya Shahada:** Ni mtu kukiri kwa neno hili, akilithibitisha moyoni mwake na kulitamka kwa ulimi wake, kwamba hakuna muabudiwa wa haki ispokuwa Allah, hivyo inahitaji kumpwekesha Allah katika ibada na kuacha ibada ya asiye kuwa Allah.

**Na Shahada ya kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah:** hivyo Inahitaji kumuamini, na kumtii kwa yale aliyo yaamrisha na kujitenga na yale aliyo yakataza na kukemea, na kumsadikia kwa yale aliyo yasema, na asiabudiwe Allah ila kwa sheria aliyo kuja nayo.

Nguzo ya pili : kusimamisha sala zilizo faradhishwa :

Na ndio nguzo kubwa ya uisilamu, sala tano zinazo saliwa mchana na usiku ndio usiano ya mja na Mola wake mlezi, anakuwa ni mwenye kumuongelesha Allah kwa siri na kumuomba, Kwa hayo, mja hupata faraja ya kiroho na kimwili kutokana na yale yanayo mfanya ni mwenye kufaulu na kupata furaha duniani na akhera.

Nguzo ya tatu : Kutowa zaka :

nayo ni sadaka ndogo iliyo kuwa wajibu kwa matajiri; ili iwe ni yenye kutakasa mali zao na kuizuwiya na majanga, na inapewa wamaskini kwa kuwafariji na kuondowa shida zao.

Nguzo ya nne : kufunga mwezi Mtukufu wa ramadhani:

Swaumu nikujiziwia kula na kunywa na kutenda tendo la ndoa (kuingiliana kati ya mke na mme) kuanzia mchomozo alfajiri hadi jua inapo zama kwa kumuabudu Allah, na Mwezi wa ramadhani ni mwezi wa tisa katika mwezi inayo endana na mchomozo wa mwezi.

Nguzo ya tano : Kuhiji

Nayo ni kukusudia nyumba ya Allah kwa ajili ya kutekeleza ibada maalumu katika wakati maalumu,Allah ameifaradhisha kwa yule mwenye uwezo mara moja katika maisha yake, waisilamu wanakusanyika kwenye idada hiyo ya hija kutokea sehemu zote kwenye ardhi tukufu(Makkah iliyotukuka), wanaume wanakuwa ni wenye kuvaa vazi la aina moja hakuna tafauti kati ya raisi na raiya na tajiri na fakiri na mtu mweupe na mweusi.

## Programu ya siku ya tisa

**45 Dakika**

za qur'ani

Inafundishwa suratul falaq yote kamili



**45 Dakika**

(Aqida(itikadi

Itafundishwa imani na nguzo zake

**Ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

# سُورَةُ الفَلَقِ

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلْفَلَقِ ﴿١﴾ مِن شَرِّ مَا خَلَقَ ﴿٢﴾ وَمِن شَرِّ
غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ﴿٣﴾ وَمِن شَرِّ ٱلنَّفَّٰثَٰتِ فِى ٱلْعُقَدِ ﴿٤﴾
وَمِن شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ﴿٥﴾

## Mpangilio wa pili : Imani

Imani ni kutamka kwa ulimi na kuitakidi(kuamini) moyoni na kutenda kwa viungo, inaongezeka kwa utiifu na hupunguka kwa mazhambi(kuasi).

**Na nguzo za imani ni sita nazo ni :** kumuamini Allah, na malaika zake, na vitabu vyake, na mitume wake, na siku ya mwishio, na kuamini makadara(alicho kipanga) kheri yake na shari yake.

**Na ufafanuzi wake ni kama ifwatayo:**

### 1.Kumuamini Allah

Nayo ni kumupwekesha Allah katika ibada ; kwa sababu yeye ndiye muumbaji na mwenye kumiliki na mwenye kuwaruzuku waja wake na muendeshaji wa kila jambo, anaye pana uhai na anaye fisha, na ni yeye wapekee anaye sitahiki kuabudiwa na wala haitekelezwe aina yoyote ile ya ibada kwa asiye kuwa Allah, kama kuomba na kutia nadhiri na kuchinja, na kwa hakika yeye anazo majina mazuri na sifa zilizo kamilika za juu, Amesema aliye takasika: {Sema : yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee, Mwenyezi Mungu ndiye mkusudiwa, hakuzaa wala kuzaliwa, wala hana anaye fanana naye hata mmoja}.

### 2.Kuamini Malaika

Kwa hakika wao ni waja watujufu, Allah amewaumba basi wakawa tu ni wenye kutekeleza ibada zake Allah, na ni wanyenyekevu kwa kumtii, na Allah akawapa kazi mbali mbali na miongoni mwao Jibril na Mikaila na Israfil Na Malakul mauti anaye wakilishwa kwa kuchukuwa roho za viumbe.

### 3.Kuamini vitabu

Nayo nikuamini vitabu vya Allah alivyo viteremsha kwa manabii wake na mitume, mfano taurati ambayo imeteremshwa kwa Mussa, na injili ambayo imeteremshwa kwa Issa, na zaburi ambayo imeteremshwa kwa Daudi rehmma na amani ziwafikiye, na suhufu ya Ibrahim na yamwisho katika vitabu hivyo ni qur'ani tukufu iliyo teremshwa kwa Muhammad rehmma na amani zimfikiye, na kwa hakika qur'an imekusanya yale yalio kuwa katika vitabu vilivyo tangulia na kufuta vitabu hivyo, Allah amejikalifisha kwa kuilinda hiyo qur'ani na itabaki kuwa hoja kwa viumbe wote mpaka siku ya kiyama.

### 4.kuamini Mitume

Allah alituma kwa viumbe vyake Mitume, wa kwanza wao(manabii) ni Nuhu juu lake rehma na amani, wakaja baada yake wengi katika manabii, miongoni mwao Nabii Ibrahim, Mussa, Isaa rehma na amani ziwe juu yao, na wamwisho wao ni Muhammad rehma na amani zimuendee, Allah amehitimisha ujumbe ulio kuwa ukipewa manabii kwa kumtuma Muhammad na akamtuma kwa watu wote basi hakuna nabii baada yake.

### 5.Kuamini siku ya mwisho :

Nayo ni siku ya kiyama ambayo Allah atakusanya siku hiyo watu wote pindi watu watakuwa ni wenye kufufuliwa kutoka makaburini mwao kwa Kukaa ama katika neema ya Pepo au taabu ya Motoni.

### 6.Kuamini makadara(alicho kipanga) kheri yake na shari yake:

Nayo nikuamini kwa hakika Allah amepangilia viumbe na kuviumba na kwa hakika yeye anatambua matendo ya waja wake, na aliyo wapangia kabla ya kuwaumba, na akaandika hayo kwenye ubao ulio hifadhika, kwa hiyo Yanayompata mtu yasingemkosa, na yaliyomkosa yasingempata.

## Programu ya siku ya kumi

45 Dakika za qur'ani

Kuhifadhi suratul falaq yote kamili kwa wanafunzi wote



45 Dakika ya kusomesha Aqidah

Ihsani(wema)

**Ukumbusho**

The lesson should be repeated on a daily basis at three intervals in order to take into account the times of all the followers. Some of them are suitable for the morning, some for the afternoon and some for the evening, and for anyone who would like to be attendance again to get more understanding.

## سُورَةُ الفَلَقِ

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلۡ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلۡفَلَقِ ١ مِن شَرِّ مَا خَلَقَ ٢ وَمِن شَرِّ
غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ٣ وَمِن شَرِّ ٱلنَّفَّٰثَٰتِ فِي ٱلۡعُقَدِ ٤
وَمِن شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ٥

## Mpangilio wa tatu : Ihsani (wema)

Nayo nikumuabudu Allah kama kwamba unamuona na ikiwa humuoni kwa hakika yeye anakuona.

Kumuabudu Allah kama kwamba unamuona: ni kuhudhurisha utukufu wake kwa sifa zake kubwa,na ukamilifu wa elimu yake kwa kila kitu, na kusikia kwake kulio kamilika kwa kila kinacho sikilika, na kuona kwake kwa kila kitu, na uwezo wake mkubwa na utukufu wake, na kumiliki kwake kulio kamilika,na upole wake na huruma wake, na hivo hivo sifa zake zote zilizo baki, Haimaanishi kwamba unahudhurisha dhati yake Allah, na hili haliwezekani kamwe, na hakuna akili inayoweza kufikiria hilo.

Na kauli yake: ikiwa humuoni kwa hakika yeye anakuona. Inamaana: unahudhurisha uchunguzaji wake Allah kwako na uonaji wake kwa matendo yako na kauli yako na kazi yako ya siri na ya wazi, na kwa hakika hakuna chochote kile kilicho fichikana kwake kutoka kwako kamwe.

Kwa hayo imani yako kwake ita ime imarika[kuzidi] na utakuwa ni mwenye kuendea vitendo vyema, na utajitahadhari na kila kitendo kisichomridhisha Mola wako Mlezi aliyetakasika.

**Swali : ni nini maana ya ibada ?**

Jibu: ibada nijina linalo kusanya kila anacho kipenda Allah na kukirizhia katika kauli na vitendo vya siri na wazi, mfano: Dua, kuunga undugu, kupenda kwa ajili ya Allah.

**Dua :** ni ibada ya kumuitajiya Allah(kumuomba), na ni mi-

ongoni mwa ibada bora, na Allah ameihimiza na kuiamrisha, amesema Alla: **{Na Mola wenu mlezi Amesema: Niombeni nitaku jibiyeni}suratu Ghaafir 60**, amesema Allah**{Na muombeni Allah katika fadhila zake}suratu nisai 32**

**Kuunga undugu:** nayo nikuwafanyia wema ndugu zako wa karibu, na iwe uungaji kwa usiyano mzuri na kwa uso wenye furaha na uchangamfu na kuzuriyana na kwa kupeyana pesa, 'amesema Mtume wa Allah juu lake rehma na amani: "ambaye anaetaka apanuliwe katika rizki yake na azidishiwe katika umri wake basi nikwake kuunga undugu wake". Ameipokea imam bukhary, kwa maana atapewa umri mrefu.

**Kupenda kwa ajili ya Allah:** ndiyo aina ya juu sana ya kupenda na ndiyo iliyo inuliwa daraja zaidi, na maana yake ni kwamba iwe sababu ya kupenda ni uchamungu na Na kumuboresha huyo anaye pendwa. Na katika hadith ya watu saba ambao Allah atawafinika katika kinvuli chake ametaja miongoni mwao: "na watu wawili wamependana kwa ajili ya Allah, wakakusanyika kwa sababu yake na wakatengana kwa sababu yake Allah".

## Programu ya siku ya kumi na moja

**45 Dakika**

- za qur'ani
- Inafundishwa suratun nasi yote kamili

**45 Dakika**

- Dakika 45 za Aqidah
- Marejeleo kamili ya visomo vilivyo someshwa vya Aqidah.

**Ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

## Qur'ani tukufu

سُورَةُ النَّاسِ

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلۡ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلنَّاسِ ﴿١﴾ مَلِكِ ٱلنَّاسِ ﴿٢﴾ إِلَٰهِ
ٱلنَّاسِ ﴿٣﴾ مِن شَرِّ ٱلۡوَسۡوَاسِ ٱلۡخَنَّاسِ ﴿٤﴾ ٱلَّذِي
يُوَسۡوِسُ فِي صُدُورِ ٱلنَّاسِ ﴿٥﴾

## Aqidah

Marejeleo kamili ya visomo vya aqidah

## Programu ya siku ya kumi na mbili

**45 Dakika**

Kuhifadhi suratu nnasi kamili kwa wanafunzi wote

Save Surat Al-Nas Complete for all students

**45 Dakika**

ya hadith

Utangulizi na utambulisho , hadith ya kwanza

**Ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote, baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

سُورَةُ النَّاسِ

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلنَّاسِ ١ مَلِكِ ٱلنَّاسِ ٢ إِلَٰهِ
ٱلنَّاسِ ٣ مِن شَرِّ ٱلْوَسْوَاسِ ٱلْخَنَّاسِ ٤ ٱلَّذِى
يُوَسْوِسُ فِى صُدُورِ ٱلنَّاسِ ٥

Zinduo

**Kisomo hiki kimekusanya:** utangulizi wa utambulisho wa hadith, na kuchaguwa baadhi ya hadith zenye maneno mafupi ya Mtume yenye maana pana, na baadhi ya uradi(dhikri).

**utangulizi:** makusudiyo ya hadithi nayo ni sunna ya nabi Muhammad sala na salamu zimuendee, nayo: ni yale yote aliyo kuja nayo nabi Muhammad, katika kauli ao vitendo ao sira yake [historia].

**Ni ipi nafasi ya sunna katika wislam ?**

Ni asili ya pili katika asili ya sheriya ya kislamu, nayo imekamilisha Qur'an na imeibainisha, sunna na qur'ani ni asili mbili inayo lazimiyana, moja aiji toshelezi na ingine, sheriya aitimiye wala aikamilike ila kwa vyote viwili pamoja.

**Na katika mambo muhimu ni kujifunza sunna ya nabi Muhammad:** nayo ni kwa sababu ya kujuwa uchambuzi ya hukmu ya dini ya kislamu na kumufata nabi Muhammad, nakujifunza fadhila na adabu na nyiradi na mambo mengine.

**Na hadithi ya nabi Muhammad ni nyingi,** basi inatutosha kutaja sehemu katika hayo, na tunaigawa sehemu mbili :

**Sehemu Ya kwanza :** hadithi zilizochaguliwa katika sunna ya nabi Muhammad zenye kukusanya maneno mengi.

**sehemu ya pili:** hadithi zilizochaguliwa katika nyiradi zilizo pendekezwa kumuabudiya kwayo Allah kwa kuzitamka.

Ya kwanza : hadithi zilizochaguliwa katika sunna ya nabi Mu-

hammad zenye kukusanya maneno mengi :

1 kutoka kwa umar bin khatwabi Allah amridhiye: amesema nabi Muhammad rehma na Amani zimuendee: “hakika matendo yanahukumiwa kwa nia, na kila mtu atapata kwa mujibu wa kile alicho kikusudia. Kwa hivyo, yule aliye hama kwa ajili Allah na Mtumbe wake, kuhama kwake ni kwa ajili ya Allah na Mtumbe wake, na yule ambae kuhama kwake ulikuwa kwa ajili ya manufaa ya kidunia, au kwa ajili ya kumuoa mwanamke(Fulani), kuhama kwake kulikuwa kwa kile kilichomuhamisha.” Kaipokea imam bukhari na muslim

**Hadithi hii ni kubwa inaelekeza**: juu ya ukubwa wa nia, na ulazima waku takasa matendo kwajili ya Allah tu, na inaelekeza kwamba kila mtu ana lipwa na kuesabiwa sawa na nia yake katika kila kitendo anacho kitenda ao kila neno anao sema, na ni katika yale ambayo yata kusaidiya kuwa na nia nzuri kila mara hata katika kazi yako ao katika misemo yako nzuri ili ulipiwe kupitiya yale.

## Programu ya siku ya kumi na tatu

**45 Dakika** za Qur'ani

- Kujifunza suratu nnasri yote kamili

**45 Dakika** za hadithi

- Kusomo na kusherehesha hadithi zingine (2,3,4 na 5)

**umbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote, baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

## سُورَةُ النَّصۡرِ

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِذَا جَآءَ نَصۡرُ ٱللَّهِ وَٱلۡفَتۡحُ ١ وَرَأَيۡتَ ٱلنَّاسَ
يَدۡخُلُونَ فِي دِينِ ٱللَّهِ أَفۡوَاجٗا ٢ فَسَبِّحۡ بِحَمۡدِ رَبِّكَ
وَٱسۡتَغۡفِرۡهُۚ إِنَّهُۥ كَانَ تَوَّابَۢا ٣

2 kutoka kwa aisha mama wawaumini Allah amridhiye: amesema Mtume Muhammad rehma na Amani zimuendee: "yule anaye tenda kitendo ambacho hakikubaliani na jambo letu kitakataliwa(kitarejeshwa)". Ameipokea imam Muslim

**Hadith hii inaelekeza juu ya:** ulazima wa kumfata nabi Muhammad sala na salamu zimuendee katika kila kitendo, na yule atakae mwabudu ALLAH kwa kitendo akikutoka kwa nabi Muhammad sala na salamu zimuendee, kita rejechwa kwa mwenye nacho (hakito kubaliwa).

3 kutoka kwa Abdillah bin amri Allah amridhiye, kasema: hakuwa Nabi Muhammad sala na salamu zimuendee, mtu muovu wala mwenye kutangaza ao kuridhia uovu, na alikuwa akisema: "hakika mbora wenu ni mwenye kuwa **na** tabiya njema". Imepokelewa na Imam Bukhari na Muslim

**Hadith hii inaelekeza:** umuhimu wa tabiya njema, na inamfanya mtu awe katika watu wazuri na awe mbora wao.

4 Kutoka kwa Abdillah bin mas'ud Allah amridhiye: amesema Mtume wa Allah sala na salamu zimuendee: "ni juu lenu kushikamana na ukweli; kwa hakika ukweli unaongoza katika wema, na wema uwongoza katika pepo, na bado mtu atakuwa ni mwenye kusema ukweli na akawa ni mwenye kutafuta ukweli mpaka akaandikwa kwa Allah ni mukweli, olewenu nauwongo, hakika uwongo unaongoza katika uwovu, na uwovu unaongoza katika moto, na bado mtu atakuwa ni mwenye kusema uongo na akawa ni mwenye kutafuta uongo mpaka akaandikwa kwa Allah ni muongo" kaipokea imam bukhari na muslim

**Hadith hii inaelekeza:** nafasi yaukweli katika uislamu na kwamba ukweli humpeleka mtu katika pepo, na Atari yauwongo na kwamba uwongo humpeleka mtu katika moto.

5 kutoka kwa Abu hurayrah Allah amridhiye: Amesema Mtume wa Allah sala na salamu zimuendee: "Alama ya mtu munafiki ni tatu: 1 anapo ongea husema uongo, 2 na anapo ahidi hatekelezi ahadi, 3 na napo aminiwa hufanya khiyana". Kaipokea imam bukhari na muslim

**Hadith hii inaelekeza:** juu ya kujitahazari na unafiki wakielemu, na baadhi ya sifa zawanafiki ambazo ni lazima kujiweka mbali nazo.

## *Programu yasiku ya kumi na nne*

**45 Dakika**

- **Quran**
  - Kuhifadhi suratu nnasri yote kamili kwa wanafunzi wote.

**45 Dakika**

- **hadith**
  - Hadithi namba 6 na 7 na visomo vingine vya hadithi

**Ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

## سُورَةُ النَّصۡرِ

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِذَا جَآءَ نَصۡرُ ٱللَّهِ وَٱلۡفَتۡحُ ۝١ وَرَأَيۡتَ ٱلنَّاسَ
يَدۡخُلُونَ فِي دِينِ ٱللَّهِ أَفۡوَاجٗا ۝٢ فَسَبِّحۡ بِحَمۡدِ رَبِّكَ
وَٱسۡتَغۡفِرۡهُۚ إِنَّهُۥ كَانَ تَوَّابَۢا ۝٣

6 Kutoka kwa ABu hurayrah Allah amridhiye amesema: Amesema Mtume wa Allah sala na salamu zimuendee: “je! mnajuwa kusengenya ni nini?” **w**akasema: Allah na Mtume wake ndio wanao jua Zaidi. Akasema: **“**ni kumzungumza ndugu yako kwa yale ambayo anayachukia”. ikaulizwa: unaona je ikiwa yale ninayo muongelea kwayo ndugu yangu anayo? Akasema: **“**Ikiwa yatakuwa kwake yale unayo zungumzia, basi bila shaka utakuwa umesha msengenya, na ikiwa hato kuwa nayo, basi utakuwa umesha mkashifu (kusemsea uongo)**”.** Kaipokea imam Muslim**.**

**Hadithi hii inaelekeza ubainifu wa maana ya kusengenya:**

Na kwa hakika yake ni kumzungumzia mtu kwa yale anayochukia akiwa hayupo, na inajulikana kuwa hakika kusengenya ni miongoni mwa madhabi makubwa ambayo ni lazima kujichunga saana ili usije ukadumbukia ndani yake.

7 Kutoka kwa Abu bakrata Allah amridhiye, Amesema Mtume wa Allah sala na salamu zimuendee: “Hivi nikujulisheni madhambi makubwa makubwa? (aka kariri swali hilo mara tatu) kumshirikisha Allah, kuwaasi wazazi wawili, na kushuhudia uongo ao kusema uongo, na Mtume wa Allah sala na salamu zimuendee alikuwa akiegemea basi akaketi, na akaendelea kurudilia mpaka tukasema: laiti angenyamaza”.

Kaipokea imamu bukhari na muslim.

**Hadithi hii imeonesha uhatari ya ushirikina:** na hakika ni lazima kujichunga saana kutokana na kuingia ndani yake, na imeonesha umebainifu pia wa ukubwa wa haki ya wazazi wawili na kujiweka mbali na kuwaasi, na kutahadharisha saana kutokana na kushuhudia uongo ao

kusema uongo, na kwa hakika hayo ni katika madhambi makubwa.

**Ya Pili**: hadithi zilizochaguliwa katika nyiradi zilizo pendekezwa kumuabudiya kwayo Allah kwa kuzitamka:

Kumtaja(Dhikri) Allah Mtukufu ni jambo linalo fanyika kwa moyo, ulimi na viungo, na Allah amehimiza kukithirisha kumtaja sana ndani ya qur'ani tukufu, Amesema aliye takasika: {Enyi mlio amini! Mdhukuruni(mtajeni) Allah kwa wingi wa kumdhukuru} suratu ahzab:41.

Na vile vile Mtume sala na salamu zimuendee amesema: "mfano wa yule anaye mtaja mola mlezi na yule asiye mkumbuka Mola wake ni kama vile mfano wa aliyekuwa hai na maiti".

## *Programu ya siku ya kumi na tano*

**45 Dakika** za Qur'ani

Kujifunza suratul kauthar yote kamili

**45 Dakika** za hadithi

hadithi za dhikri, wanafunzi wazihifadhi wanafunzi wote

**ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

## سُورَةُ الكَوثَر

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِنَّآ أَعۡطَيۡنَٰكَ ٱلۡكَوۡثَرَ ١ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنۡحَرۡ ٢
إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ ٱلۡأَبۡتَرُ ٣

**Kumtaja Allah kuna aina nyingi, miongoni mwayo:**

**Aina ya kwanza:** kumtaja Allah kwakila wakati**.**

**Kama kusema:** SUBHANALLAH (ametakasike Allah), WAL HAMDULILLAH (nashukuruni ni zake Allah), WALAA ILAHA ILALLAH (na hakuna hakuna muabududiwa ila yeye Allah, WALLAHU AKBAR (na Allah ni mkubwa mno, hakuna uwezo wala nguvu ila zake Allah, Mtume sala na salamu zimuendee kasema: "maneno mazuri yanayo pendwa Zaidi kwa Allah ni 4: SUBHANALLAH (ametakasike Allah), WAL HAMDULILLAH (nashukuruni ni zake Allah), WALAA ILAHA ILALLAH (na hakuna hakuna muabududiwa ila yeye Allah, WALLAHU AKBAR (na Allah ni mkubwa mno".

**Nakusema : "**hakuna uwezo wala nguvu ila zake Allah" ni azina miongoni mwa azina ya peponi

**Na amesema sala na salamu zimuendee:** "atakae sema SUBHANALLAHI WABIHAMDIHI (ametakasika Allah na shukurani nizake yeye Allah) kwa siku mara mia moja, ata semehewa madhambi yake hata iwe mfano wa povu ya bahari".

**Na akasema Mtume wa Allah sala na salamu zimuendee:** "maneno mawili ni yenye kupendwa kwa Allah, mepesi kwenye ulimi, na ni nzito kwenye mzani: SUBHANALLAHI WABIHAMDIHI SUBHANALLAHIL A'DHWIIM (ametakasika Allah na shukurani niza yeye Allah, ametakasika Allah mtukufu)".

**Aina ya pili :**Kumtaja Allah asubuhi na jioni :

**Kusoma sura tafauti:** suratul ikhlas na falaq na annas, mara tatu, asubuyi na jioni, na kabla yaku lala.

**"**LA ILAHA ILALLAHU WAHDAHU LA SHARIKALAH, LAHUL MULKU WALAHUL HAMDU WA HUWA A'LA KULI SHAY-IN QADIIR(hakuna

apasae kuabudiwa kwa haki ila yeye Allah peke yake ana mshirika wake, ufalme ni wake na shukurani zote nizake  na yeye ndiye mwenye uwezo wakila kitu)" inakaririwa mara kumi, na asubuyi pia.

"SUBHANALLAHI WABIHAMDIHI (ametakasika Allah na shukurani nizake yeye Allah)" mara mia moja, nayule atakae sema hayo, hakuna mtu atakae kuja na kilicho kuwa bora zaidi ya hayo aliyo yasema ila yule atae sema mfano wa hayo ao akazidisha Zaidi ya yale alio yasema yeye.

"BISMILLAHI LADHI LA DWURU MA'SMIHI SHAY'UN FIL ARDWI WALA FI SAMAA, WA HUWA SAMIU'L A'LIIM" (Kwajina ya Allah ambaye aizuru pamoja na jina yake kitu chochote katika dunia wala katika mbingu  na yeye ana sikiya na anajuwa) mara tatu, yeyote ataesoma hakito mzuru chochote kile.

Kusoma ayatul kursiyi asubuhi na jioni na wakati wakulala na mwisho wa kila sala.

Kusoma aya mbili za mwisho ya suratul baqara asubuhi na jioni.

Na inapendeza  useme :  "BISMILLAH (kwajina la Allah)" kabla ya kushika udhu(kutawadha)  na kabla ya kuingiya chooni na kabla yakula na kunywa maji, na unapo ingiya muskitini na pindi unapo toka muskitini na wakati unata kuingiliana na mke wako(mme)na mengineo.

Na ukimaliza kula na kunywa utasema:  ALHAMDULILLAH (namshukuru Allah).

Ina pendeza kuomba msamha kwa Allah kwawingi kwa kila wakati na huko ni katika kumtaja Allah, basi utasema: ASTAGHFIRULLAH ASTAGHFIRULLAH (nakutaka msamaha ewe Allah nakutaka msamaha ewe Allah) ... ao unasema:     RABBIGHFIRLII WA TUB A'LAYYA Ewe Mola wangu nisamehe na utubu kwangu, na mengineo.

**Omba kwa wingi katika kila wakati, kwa sababu Qur'ani na sunna [hadithi] vimehimiza sana watu waombe msamaha kwa wingi.**

## *Programu ya siku ya kumi na sita*

**45 Dakika** — Qur 'an

- Kuhifadhi suratul kauthar yote kamili kwa wanafunzi wote

**45 Dakika** — za hadith

- Marejeleo ya visomo vya hadith vyote kamili

**Ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

## Qur'ani tukufu

سُورَةُ الكَوثَرِ

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِنَّآ أَعۡطَيۡنَٰكَ ٱلۡكَوۡثَرَ ١ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنۡحَرۡ ٢

إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ ٱلۡأَبۡتَرُ ٣

## Hadith

Marejeleo ya visomo vya hadith vyote kamili

## *Programu ya siku ya kumi na saba*

**45 Dakika**

- ya qur'ani
- Suratul asri yote kamili na kuihifadhi hiyo hiyo siku

**45 Dakika**

- thaqafatun islamiyya (utamaduni wa kiislamu)
- Kujumuisha wa dini ya kiisilamu katika ujumbe wake na kuzungumzia kiufupi ukamilifu wa dini ya kiislamu na uwepesi wake.

**Ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

## سُورَةُ العَصۡرِ

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

وَٱلۡعَصۡرِ ١ إِنَّ ٱلۡإِنسَٰنَ لَفِى خُسۡرٍ ٢ إِلَّا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ
وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ وَتَوَاصَوۡاْ بِٱلۡحَقِّ وَتَوَاصَوۡاْ بِٱلصَّبۡرِ ٣

**Na hizi ni baadhi ya amri ilizo ziamrisha uisilamu, na baadhi ya makatazo iliyo weza kuyakataza bila ya ufafanuzi, na vile vile hayo mambo yanaitaji ubainifu:**

**Kipengele cha kwanza : katika yale uislamu imeweza kuyaamrisha:**

Kutekeleza ibada kwa ajili ya Allah(ikhlas), kulinda amana, kuwatendea wazazi wawili wema, kuwa na tabia njema, kuunga undugu, kutekeleza ahadi, usafi, upole, kuitikia wito, kujiteremsha, uvumilivu, kufuga ndevu, kuunga undugu wa kiislamu, kumtendea wema jirani, kumkirimu mgeni, kutoleana salamu, kulishiza chakula, kuwapenda waisilamu, kumnusuru aliye dhulumiwa, kuwahurumia watu wote.

Kipengele cha pili : na katika yale uislamu imeweza kuyakataza:

Kumshirikisha Allah, kuacha swalah, kuwakosea wazazi wawili, uchawi, kunywa pombe na uvutaji wa dawa za kulevya, kuteta, kula riba, kula mali ya yatima, kuwatupia maneno mabaya wanawake walio jilinda kutokana na uchafu wa zina, kusengenya, kuuwa nafsi bila hatia, kukata undugu, kula vya haramu, uzinifu, kuingiliana kwa nyuma, rushwa, wizi, kulaaniana, kufanyiana khiyana, kamari.

**Na mengineo yenye kumu fanya mtu awe kama mnyama hajiimizi na kitu ila tama yake nama tamaniyo yake tu.**

**Kiufupi kutokana na ukamilifu wa dini ya kiislamu na upole wake:**

Hakika iyi dini ni dini ambao kairiziya Allah kwa viumbe wake, dini nyepesi tena rahisi sana, hakuna uzito ndani yake wala usumbufu, ai mulazimishi yule mwenye kuikubali yale asio

ya weza, dini ambayo msingi wake ni ibada ya Allah pekeyake na nembo yake ni ukweli.

Maamrisho yakislam yote ni uwadilifu, ina waita katika tabiya nzuri, nakuwaita katika ukweli na kujiziwia na kutenda maovu na uwadilifu, nakuhifazi ma mapatano, na ku kutekeleza amana za watu, na kukirimu wageni, na kujipamba kwa tabiya nzuri, nakumpa mwenye haki haki yake awe mkubwa ao mtoto mwanaume ao mwanamke, piya inawaita kupata maisha mazuri katika uwadilifu na usawa,wala ai amrishi ispokuwa yale mazuri katika dunia na yale yama fanikio,wala haikatazi ila yenye kuleta uzito namazara kwa watu, maamrisho yote katika dini iko kadir yauwezo wamtu ai muamuru yale awezi, na akisau ao ajuwi, ao kakoseya ana samehewa kwa sababu iyi dini ina jengeka kwa uruma.

**Na katika ukamilifu wa uislamu :**nikule kumpa mwanamke nafasi kubwa, na haki kamili kama mwanaume.

Uislamu ni dini kamili yenye kukusanya kila kitu haiku ghafilika kutokana na haki za mwanamke katika sheria zake na hukumu zake, uislamu uli kuja kunyanyuwa nafasi ya mwanamke, nakumkirimu kama vile ajawi kirimiwa na dini ingine ao utamaduni ungine kabla ya dini ya uislamu, hakika wanawake katika uislamu ni ndugu wa karibu zaidi ya wanaume, na mwanamke naudogo wake lakini uislamu unampa hukmu yake, ambayo inalinda haki yake na utukufu wake, tangu utotoni mwake uislamu umemlindia haki ya kunyonya, matunzi mazuri na malezi bora, Kisha alipokua, alilindwa vyema na familia yake, na msimamizi wake amekuwa karibu nae kwa uangalizi wake, Hakuna mtu aliyeruhusiwa kumnyooshea mkono kwa kumwaribiya maisha yake, Na alipoolewa, Allah alifanya agano(mapatano) lake la ndoa kuwa agano(mapatano) zito, Na akamuamuru mume

wake amheshimu na kumfanyia wema, Na pindi alipofikia kuwa mama, kumheshimu ilikuwa moja ya mambo ya lazima zaidi, na haki yake ikawa ni yenye kuambatanishwa na haki ya Allah, na vile vile alipofikia kuwa dada ao mama mdogo au bibi(taté), kwa hakika mtu anakuwa ni mwenye kuamrishwa kuunga undugu wake, kumheshimu na kumfanyia wema.

uislamu uli mukirimu mwanamke pindi ilimuwekea haki ya kumiliki, kuajiri, ku uzisha, kununua na mengineo, na uislamu umempa mwanamke haki yake ya kusoma, bali katika ilimu kuna iliyo kuwa lazima juu ya kila muislamu mwanaume na mwanamke, na miongoni mwa utukufu uliyo kamilika aliyo pewa mwanamke katika uislamu kwamba Allah amemuwekea sheria ambayo inamulinda na kumuhifadhi kutokana na ndimi chafu yenye kumtupia maneno mabaya, na macho mbaya na mkono mbaya ya kutaka kumharibu, sheria ika muamrisha kuvaa hijabu(vazi kamili ya kumuenea mwanamke mwili wake wote), na kuepuka kuji changa na wanaume, Na mambo mengine yanayo linda utu wake.

Na mwanamke pia katika sheriya ya uislamu anayo haki katika kurithi, hakuna yoyote anaweza kumziwiya kwayo, basi mwanamke wakiislamu amekirimiwa katika hali zote na maisha yake mengine, ana ishi katika ulinzi wa wazazi wake, na utunzaji wa mume wake, na katika wema ya watoto wake

Na uislamu ume muhalalishia mwanamke kuachana na mume wake ikiwa atamzulumu na kumfanyiya mabaya na kuishi naye vibaya, nani kwake yeye mwanamke Kupatana na mume wake kuhusu jambo Fulani kama kumrejeshea mahari alitowaga na baada ya hapo waachane nae.

**Shauri yaku maliziya kwako :**

Ndugu yangu mpendwa pindi Allah alipo kukirimu na kuku

fadhilisha zidi ya wengi katika watu na kukuchaguwa kwenye neema kubwa hii, neema ya kukuongoza katika dini ya uislamu, ambayo kwa sababu yake utapata mafanikio katika dunia na akhera.

**Tuna kuusiya kwa usiya mwingi, miongoni mwazo zilikuwa muhimu Zaidi ni:**

**Ya kwanza:**ni lazima kwako kuilinda iyi neema na kuogopa isi kuondoke, na umuombe Mola wako kila mara uthibitisho kwalo mpaka kufa, kwa hakika Mola wako kakuamrisha hayo, Amesema aliye tukuka: {Enyi mlio amini! Muogopeni Allah ukweli wa kumuogopa wala msife ila nanyi ni waislamu wakweli} Suratu ali Imran:102.

**Ya pili:** Kuwa mwangalifu usijione wewe ndiye mbora na ujitenge na matamanio ya nafsi, kwani unaweza kupotea kutoka katika Uislamu kwa mtihani unao jitokeza kwako, kwa hivyo huna budi kumuomba sana Mola wako Mlezi uthibitisho, ukisema: “Ewe Mwenye kugeuza nyoyo thibitisha moyo wangu kwenye dini yake”. Amekuwa kiigo chako Nabii Muhammad sala na salamu zimuendee akiomba iyi dua kwa wingi, na Allah ametaja miongoni madua ya waja wake wema {(Na hao husema): Mola wetu Mlezi! Usizipotoze nyoyo zetu baada ya kwisha tuongoza} suratul ali imrani :8

**Ya tatu:** pupiya kufanya sababu yakufanya kuthibiti katika dini ya uislamu, naya muhimu sana ni:

Kufata mamrisho ya Allah na kuachana na yale yote aliyo yakataza.

Kulazimiana kudumisha swala kwa wakati kwa wakati wake

Kuzidisha kuomba dua kwa wingi, na kumtaja Allah(dhikri), na kuomba msamaha.

Kusoma kiwango fulani katika Qur’ani tukufu kila siku, na hata akikariri zile sura fupi; kwa sababu Qur’ani ni ponyio kwa watu ka-

tika maradhi ya matamanio na shubuhati (mambo ya kutatanisha).

Nijulako kuwa nawarafiki wazuri, kwa sababu mtashauriyana nao katika ukweli nasubra.

Niju lako uwe kila mara una hisi kwamba mola wako ana kuona na yeye ndiye anae kulinda na kuku saidiya.

**Ya nne**: jiweke mbali nakila Kitakacho kuondowa katika uislamu, kwa kuogopa kuiacha uislamu ukapeleka nafsi yako katika adhabu itokayo kwa Allah, Na mojawapo ya sababu muhimu zaidi za upotoshaji ambazo unapaswa kuepuka ni:

Madhambi madogo na makubwa

Kurafikiana na warafiki wabaya, na wale ambao wanaweza kukushawishi ukaanguka katika uovu.

Kupuuzia swala, kuifanyiya uvivu na kuichelewesha na kuisiali nje ya wa wakati wake.

Kuwazarau watu na kuwanyima haki zao, na kuwafanyiya uadui, na maaudhi.

Kula mali ya haramu ; kama mali ya wizi, ya kudanganya, riba na mengineo.

**Ya tano:** uwe mwenye huruma kwa watu wote, malengo yako kila mara iwe ni yenye kuwaokowa Katika njia ya moto kuwa peleka kwenye njiya ya pepo, na uwe mwenye kutowa ushauri kwa mwenye kuitaji ushauri, kwaku zingatiya kauli ya Nabii Muhammad sala na salamu zimuendee: "Ambaye atakae ita kwenye uongofu atakuwa na malipo kama malipo ya wale watakao mfuata na hato punguza katika malipo yao chochote". Na Allah atakuandikia malipo sawa na malipo yule mwenye kusilimu kwa sababu yako, na malipo ya kila yule atakae silimu kwa sababu yao paka siku ya kiama, ina kuwa kwako ni matendo yenye kwendeleya baada ya kifo chako kama vile sadaka yenye kuendeleya.

## Programu ya siku ya kumi na nane

### Marejeleo ya programu yote kwa waongofu wapya wote

| Muda | Somo | Maelezo |
|---|---|---|
| 20 Dakika | qur'ani | Kurejelea suratul faatihah, al ikhlas, al falaq, annasi, al a'sri, al kauthar na annasri. |
| 20 Dakika | Aqidah | Kurejelea mipangilio ya dini, nguzo za uislamu na nguzo za imani. |
| 20 Dakika | fiqhi | Itarejelewa kisomo cha Twahara na Swala. |
| 20 Dakika | hadith | Itarejelewa hadithi za Adhkar(dhikri). |

**Ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

| Yanayo hitajika | Mada | Muda |
|---|---|---|
| 1.Ni nini uislamu ?<br>2.Nabii gani ambaye Allah kamtuma na ujumbe wa uislamu ?<br>3.ni matendo gani ambayo uislamu uli amrisha ?<br>4.ni matendo gani ambayo uislamu uli kataza ?<br>5.Ni nini qur'ani tukufu? Na ni malipo gani ya kuisoma ?<br>6.soma suratu hizi: (al-fatihat, al-ikh-las, al-falaq, an-naas, al-asri, al-kauthar na annasri)<br>7.Simama utawaze na uswali.<br>Kurekebisha makossa ikiwa yatapatika-na.<br>8.Kila swala ina rakaa ngapi?<br>9.Ni nani Mola wako mlezi? na ipi dini yako? na nani Nabii wako?<br>10.Nguzo za uislamu ni zipi ?<br>11. Ni nini hadith ?<br>12.Ni ipi dhikri ya asubuhi na jioni ? | Tathmini ya Muislamu mpya<br>mtihani wa kujibu kwa mdomo<br>kwa wana-.funzi wote | Saa moja na nusu |

## Siku ya ishirini na ndiyo ya mwisho

**Saa moja na dakika 30 za kurejeleya**

yale yalio onekana kama madhaifu kwenye siku ya 19 pamoja naku rejeleya kitabu chote

Na mwisho wadarasa mwalimu ataandika majina ya wanafunzi walio jipambanua kwa bidii ya kusoma na wakawa na alama nzuri na anwani zao, na namba zao za simu zao; ili kuwasiliana nao na kuwaandikisha katika za daura za kielemu zijazo.

**Ukumbusho**

Ni lazima kurudiliya somo kwa siku katika vipindi vitatu tofauti kwa kuzingatia nyakati ya waingia dini wote baadhi yao muda wa asubuhi ndio unayo nasibiyana nayo na baadhi yao muda wa adhuhuri na baadhi yao jioni, na ili awezeshwe kila anaye taka kuhudhuria kwenye kila kipindi cha somo na ili aweze kufahamu Zaidi.

## *Maswali yanayo jirejesha kila mara kwa waislamu na wasiyo kuwa waislamu, na mujibu yake*

### Ni nani Allah ?

Allah ni yeye mumbaji mkubwa, aliumba dunia yote, na yeye ndiye anastahiki kuabudiwa peke yake bila kumshirikisha, na yeye ndiye mwenye rehma mwenye kurehemu na uruma na ni mpole na mukarimu.

Na anawahurumiya waja wake na ana wafaninya wema naku waruzuku nakuwa jibiya dua zao, na anawakasirikia wale ambao wana mukufuru, nawale ambao wana kataa kuti mamrisho yake na kuacha yale aliyo yakataza.

Na Alla aliumba viumbe viote kwajili wamuabudu nakumpwekesha, kama vile yeye ni muumbaji peke yake ndo vile vile ni Mola mlezi na Muabudiwa peke yake aliye takasika.

### Ni nini maana ya uislamu na ni wakati gani uislamu ulianza ?

Uislamu ni kunyenyekeya na kujisalimisha kwa Allah

Nayo nikushahidiliya ya kwamba hakuna muabudiwa wa haki ila yeye Allah na Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake, na kusimamisha swala, na kutowa zaka, na kufunga mwezi wa ramadhani, na kwenda hija kwa mwenye kujiweza.

Na muislamu ni yule ambaye waislamu wamesalimika kwa ulimi wake na mkono wake, na asimuudhi yeyote yule bila haki.

Na uislamu umeanza pindi Allah alipo mtuma Nabii wake Muhammad sala na salamu zimuendee kwa watu wote. Na Allah alimtuma kabla ya miaka Zaidi ya 1400.

Na uislamu bado ungali nazagaa na kuwa mkubwa zaidi tangu

wakati ule mpaka leo, na waislamu leo idadi yao inakuwa zaidi ya miliari na nusu, ashukuriwe Allah.

**Ni ipi miujiza za Mtume Muhammad sala na salamu zimuendee?**

Mtume sala na salamu zimuendee anazo miujiza mengi sana, yawezekana kuyasoma ndani ya vitabu vinavyo elezeya miujiza na matukio katika wakati wake, lakini mujiza wake mkubwa ni qur'ani tukufu ambacho kiko mbele yetu, maneno ya Allah aliye takasika, nayo ni mujiza wenye kubaki mpaka siku yakiyama.

Kwa hiyo, Qur'ani Tukufu ilitoa changamoto kwa mtu yeyote kuleta mfano wake au mfano wa surah moja kutoka humo, Alla anasema: {Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyo mteremshia mja wetu basi leteni sura moja ya mfano wake, na muwaite mashahidi wenu badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli.}. Suratul baqarat:23

Na amesema aliye tukuka {Sema: Wangeli kusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'ani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao}. Suratul israa:88

Na tangu ili teremshwa qur'ani mpaka leo haja weza mtu wala hato weza yeyote yule kuleta mfano wa qur'ani wala mfano wa surat, na hili laonesha kwamba siyo maneno ya watu, na hakika yake ni muujiza mkubwa yenye kubaki milele.

Na ndani ya qur'ani muna elimu na habari na visa, na maubiri, na maalama zenye kuonesha ukubwa wa ALLAH, na kuonesha kwamba kweli ni kitabu kilicho toka kwa Allah aliye takasika.

**Qur'ani ime toka wapi ?**

Qur'ani tukufu imetoka kwa Allah, nayo ni maneno ya Allah ya wazi, alimteremshiya Mtume wake Muhammad sala na salamu zimuendee, ili awaonye kwayo viumbe wote na awaite kwenye dini ya kiislamu.

### Je, uislamu ume tangazika kwa vita ?

uislamu hautangazike kwa vita, bali kwa rehma na uadilifu baina ya watu, uislamu ni dini ya rehma na uadilifu, na inaendana na umbilo ya kibinaadamu, ndiyo kwa maana watu wanaikubali kwa wingi, kwa sababu inaendana nao kwa fitra yao safi.

Na istoria inashuhudiya kwamba uislamu ulisambaa baina ya watu kwa kupenda kwao, na mpaka leo watu wana kubali uislam pamoja na uzhaifu iliyo na waislamu, bali uislam leo ni dini inayo kubaliwa kwa wingi kushinda madini yote.

### Je, waislmu wana amini kwamba issa[ yesu] ni mungu?

Waislamu wana amini kwamba issa [yesu] ni nabi wa Allah na muja wake, na mtume wake, na mama yake Mariam Amani ya allah iwe juu lake ni msafi mkweli, kwa hiyo wao ni watu miongoni mwa waja wa allah mtukufu.

### Ni ipi dini ya manabii wote ?

Dini yama nabi wote ni kumpwekesha Allah peke yake, hata kama majina ya madini yao itatofautiyana, ispokuwa wote wana linganiya kwa kumwabudu tu Allah peke yake bila kumshirika.

Na kumpwekesha Allah ndiyo uislamu na kunyenyekeya katika mamrisho ya Allah, kwa hiyo asiabudiwe yeyote ispokuwa tu Allah, wala kuombwa ispokuwa tu Allah, na yeye ndiye mumbaji pekeyake, na ni mwenye kuruzuku, na mwenye kuleta uzima na kifo.

Na hii ndiyo dini ya manabii wote rehma na amani iwaendeye wote.

Na waislamu wanaamini manabi wote wa allah.

### Je! Inajuzu kusali kwa lugha ingine isiyo kuwa ya kiarabu?

Hapana, haijuzu na wala haisihi kusoma qur’ani ispokuwa kwa lugha ya kiarabu; kwa sababu kile kinacho somwa kwa lugha

isiyo kuwa ya kiarabu haitwi qur’ani na sivingenevyo hiyo inaitwa tafsiri ya qur’ani. Lakini yule asiye weza kuitamka hiyo qur’ani kwa kiarabu nikwake kusema na kukariri: “SUBHANALLAHI WAL HAMDULILLAHI WALAA ILAHA ILALLAH WALLAHU AKBAR”. Na inajuzu kuikariri peke yake

hakuna tatizo kuitamka kwa lugha yake mpaka pale atakapo jifunza lugha ya kiarabu, na hivyo hivyo kwenye nguzo zingine za swala, akiwa kwenye rukuu ao sijida na kwenye kikao cha tashahud na penginepo aseme maneno yale kwa kiarabu na asipo weza kuyatamka kwa kiarabu basi nikwake kuyatamka kwa lugha yake mpaka pale atakapo jifunza.

### Je, ina juzu kusaidiana na wasiyo kuwa waislamu?

Nam, ina juzu kusaidiana na wasiyo kuwa waislam katika yale ambayo ina faida na kheri (katika mambo mazuri). Amesema allah mtukufu: (na saidianeni katika wema na uchamungu, wala msisaidiane katika zhambi na uadui). Surat maidah:2

Na amesema mtukufu: (mwenyezi mungu hakukatazeni na wale ambao hawakupiganisheni vita katika dini, wala hawakutoeni katika nyumba (nchi) zenu kuwafanyiya wema na uadilifu; hakika allah huwapenda waadilifu). Surat mumtahinat:8

Na mana ya aya: hakika Allah hawakataze waja wake kusaidiyana kwa wema na uadilifu pamoja na wale wasiyo kuwa waislamu katika yale ambayo ina kheri na manfaa kwa wote, lakini ikiwa ndani yake kutapatikana zhulma na uadui hapo haijuzu kujiunga na wao.

### Kwa nini wislamu unaharamisha nyama ya nguruwe?

**u**islamu ni dini ya Allah muumbaji mtukufu, kwa hiyo Allah ndiye menye kuamrisha kile anacho kitaka, na kukataza kile anacho kitaka, na ana halalisha kile anacho kitaka, na kuha-

ramisha kile anacho kitaka, na sisi ni waja wake tunasikiya na kunyenyekeya katika maamrisho yake na makatazo.

Allah ameisha haramisha kwa  waja wake waislamu kula nyama ya nguruwe na mengineo katika ma aina tofauti ya nyama, na akawahalalishiya aina nyingine nyingi katika manyama

Na science ya leo inaisha hakikisha kwamba nyama ya nguruwe inaleta mazhara kwa binadamu.

Djapo kuwa science hainge thibitisha hao, ina tosha kwamba Allah ameisha haramisha ile nyama ya nguruwe, na ndiye mdjuzi wa kujuwa yaliyo na faida kwa mtu na yale yatakayo mzhuru mtu, na Allah ndiye aliumba watu na anajuwa yalio kuwa mazuri kwao.

### Pepo na moto viko wapi?

Pepo ni malipo ya Allah kwa waja wake waislamu, na moto ni malipo ya Allah kwa waja wake wenye kumu kataa na kukataa maneno yake   namitume wake.

Pepo na moto ni viumbe katika viumbe vya Allah

Na pepo iko mbinguni, nayo ni kubwa sana hakuna mwenye kujuwa upana wake ispokuwa tu peke yake Allah.

Ama moto ipo hapa duniyani lakini sehemu haijulikane, lakini sisi tunaamini kwamba ipo kwa sababu Allah ka tuambiya kuhusiyana nayo.

Na hii duniya ni kubua sana, wala mtu, pamoja na elimu ginsi inavyo endelea, hawezi kujuwa elimu yote ila tu sehemu ndogo sana.

### Je, ina juzi kuomba manyota ili nvua inyeshe ?

haijuzu kuomba nyota ao vitu vingine, wala haijuzu kuomba nvua kupitiya nyota ao vitu vingine.

Allah pekeyake ndiye anastahiki kuteremsha nvua, na yeye pekeyake ndiye mwenye kuruzuku...

Na nyota ni viumbe miogoni mwa viumbe vya Allah, avi miliki manfa ao mazara, Allah pekeyake ndiye mwenye mazuri na riziri inapatikana mikononi mwake.

Na hivyo hivyo kuomba nyota na kutafuta msaada kupitiya nyota inahesabika kuwa ni shirki (kumuchanga Allah na viumbe) kwa hiyo haijuzu, na hakika uislam umeisha haramisha kuomba nvua kupiya nyota ao mengineo.

**kwa nini ni lazima kushika uzhu {ablution} kabla ya kusali?**

uzhu ni ibada iliyo amrishwa na uislam wakati wa kusimama kusali.

Ni kama vile swala ni ibada ina hikma yake, na hivyo hivyo uzhu piya ni ibada ina hikma yake.

Na uzhu ni kuosho viuongo maalumu, katika uzhu kunapatikana maandalizi ya kiroho kwa ajili ya sala, na kujikurubisha kwa kusali na twahara na usafi ya viungo vya nje, kwa ajili ya mtu atafuta usafi na twahara ya moyo na roho yake.   Wake

**Je, uislam inajuzisha kuowa wanawake Zaidi ya moja?**

**uislam inajuzisha kuowa wanawake** mpaka wa nne ili ahifazi eneo ya familia yake, na ili mwanaume asitafute mwanamke mwingine wa haramu.

Kama vile, bila shaka wanawake katika hali ilivyo, ni wengi saana kushinda wanaume ginsi historia inavyo endelea, kwa hiyo uislam ilikuwa imelinda hii djambo.

Na uislam pindi ilipo ruhusiya kuowa wengi iliruhusiya kwa sharti ya kujiweza kuowa, na uadilifu kati ya wanawake, na kama hatoweza, basi uislam umemuharamishiya kuowa wengi.

### Je, ni wajibu kuvuwa viato wakati wa kusimama kusali?

Ndiyo ni wajibu kuvuwa viato kama ni vichafu vya najisi, na ikiwa kama siyo vichavu basi siyo wajibu kuyavuwa, kwa hiyo hiyo imeruhusiwa kusali navyo kama ni visafi.

Lakini ikiwa Sali ni ndani ya muskiti na muna misala (tapies) bora ni kuvuwa viato kwa hali yeyote ile.

### kwa nini islam ina kataza kunua pombe ao aina yote ya ulevi?

Dini ya kislam ilikuja kwa ajili ya kulinda masilahi (mazuri) ya mtu, na masilahi ya muhimu saana ni yale ambayo islam ina amrisha kuilinda: akili na nafsi na heshima na mali.

Na katika yale ambayo sheriya ya kislam inaya kariri saana ni kwamba ilikuja kuleta masilahi na kuyakithirisha, na kuondoa mabaya na kuyapunguza, kwa hiyo yale yatakayo kuwa yenye manufaa (mazuri) ao manufaa (mazuri) yake itazidi itakuwa ni halali, na yale mabaya yatakuwa yenye mazhara ao mazhara yake itazidi yatakuwa ni haramu, na pombe inatokana na hii sehemu ya pili pasina khilafu.

Kwa sababu pombe unaondowa akili ya mtu, na huenda mtu anaweza kufanya mabaya mengi katika hali ya ulevi, na hiyi ni kinyume na mazuri ya kiujumla kiupekee ambayo ni lazima kwetu kuyalinde.

Na ulevi unakusanya maovu mengi ambayo ilistahiki nabi wetu aliongeleye kuhusu ulevi< ulevi ni mama ya mabaya yote>.

Na hii imetokeya kweli, kwa hiyo mwenye kunywa pombe hutokwa na kili, basi huwa anafanya maovu kwa rahisi, na huenda inasababisha kupatikana na ajali kubwa kubwa, mfano ajali ya njiani na kuanguka kutoka juu na mengineo.

### Kwa nini islam inaharamisha kutumikisha riba katika pesa?

Uislam inaamrisha kuhifazi mali, nakuifanya iwe nyingi, na kwenda kuitafuta katika njiya nzuri yaki sheriya ambayo haina mazhara ndani yake ao mazhara kwa mtu, basi Allah akahalalisha ku uzisha na ku nunuza, na akaruhusiya kufanya viashara na kukopa, hivi vyote ni malango iliyo ruhusiwa kwa kupata pesa, kwa sababu kupitiya mali ndiyo maisha ya watu inapata uzima na duniya inaimarika.

Lakini uislam ina haramisha riba kwa njiya zote, na sababu ya ku haramishiwa ni kwa sababu katika riba kuna mazhara kwa watu, na kuharibu djami, na inaleta uadui.

Na kutumikisha riba inazhuru kwa wenye kuwa na kipato kidogo, na inafanya viashara yao kuwa mbovu, na katika upande mwengine inawazidishiya wenye kuwa na pesa wazidi kupata pesa bila tabu ao kufanya biashara ao ku uzisha.

Hakika islam kuharamisha riba ni kwa sababu ya kukataza ku zhulumiyana, kwa sababu katika riba ni kubeba mali ya watu bila kubadirishana, na kula pesa ya watu kwa uongo, na vilevile ku chukuwa pesa ya riba ni kubeba pesa bila tabu yoyote wala juhudi, na yeye ana chukuwa pesa kwa tabu ya mwingine, bila yeye kuweka mali yake katika njia kufaidika ao hatari yoyote.

Kama vile uislam pindi iliharamisha riba na vilevile inakataza kukaa bila kutumika na kuto kukimbilia kufanya kazi, na kuto kutafuta katika njia ya halali, kama vile viashara, kulima, viwanda, na mengine katika mali, jambo ambalo litakuwa sababu ya kuhakikisha malengo ya kuimarisha dunia, nayo ikawa haipeleke watu kuamiliana kwa riba.

Na uislam inahiza watu kufanya wema na kheri na mambo mazuri kwa watu, na riba inapelekeya watu kukata undugu, na kuto kusaidiana baina yao na kuto kuondoleana mazito.

Ndo maana uislam inaharamisha riba na kuizuwiya, kwa ajili

ya kuhifazhi maisha ya watu na mali yao.

Kwa nini uislam ina harahmisha zina inje ya ndoa ?

Uislam unaharamisha zina kwa njiya yoyote inje ya ndoa, kwa sababu kuna faida na masilahi ya wanaadamu wenyewe, na mwiongoni mwayo:

1- hiyo ku haramisha ina afikiana na umbilo ya ubina adamu ambayo Allah kauweka ndani yao, kutokana na wivu ya kiheshima, ni binadamu gani ambaye amekubali kuwa mke wake ao mtoto wake wa kike ao mama yake ao dada yake wawe ni viashara vya watu kwa bure, basi atakuwa amerizhiya nafsi yake kuitiya katika tabaka ya baazhi ya wayama.

2-kukataza kuchanga nasabu, sababu anaye ruhusiya zinaa basi ameisha ruhusiya kuingiza mtoto asiye kuwa wa mgongo wake katika familia yake na jamaa yake.

3-inahifazi familia na maisha ya kijamii, kwa sababu zina huwa inaharibu nyumba na kuibomoa, mwanaume akichugua mke wa inje, na mke akichugua mme wa inje, hakuna shaka katika hivyo vitendo vitaharibu familia na kuyaachanisha.

4-inakinga kutokana na magonjua, ambayo ndiyo azhabu ya Allah kwa wenye kufanya ile machafu, wala haifichame kwa kuangaika ya wengi katika watu wenye kufanya zina kutokana na magonjua yanya hatari mno, mfano kaswende, kisonono, ukimwi yenye kumaliza milioni ya watu na bado wengi wanasibiwa na yale magonjwa, kuanziya mwaka wa 2006 ilifikiya wingi wa wenyewe walipatikana na iyi magonjua 45 milioni, na wale waliyo fariki kwa sababu ya yale magonjua idadi yao ni karibiya 20 milioni, na idadi karibiya 301 milioni ni natija inayo ungana na sababu ya ile magonjua.

Na inazingatiwa kwamba iyi ukimwi ni sababu kubwa yakifo

katika inchi yaki Africa, na piya ni sababu ya inne ya kifo katika dunia nzima.

Kwani mwenye akili gani itarizika kwa kusambaa kwa iyi magonjwa katika jamii?

Kasema nabi muhammud: "**haiwe kuzihiri machafu katika watu kamwe na waifanye wazi, ispokuwa Allah atawaleteya magonjwa ya kuambukiza (epidemie) na njaa ambao haikuwa katika wale walio pita kabla yao**". Na imeisha tokeya yale alituambiya nabi Muhammad.

5-kuhifazi heshma ya mwanamke, kwa sababu ku halalisha zina ina maanisha kumvua mwanamke heshima yake, na kumfanya awe viashara visivyo kuwa na faida, na uislam ilikuja kukirumu watu na hasa zaidi kumukirimu mwanamke, baada ya mwanamke kuwa ni mzhalili na haeshmiwe

6- kukataza kusambaza maovu, kwa sababu zina ni miongoni mwa vitendo vinavyo sambaza maovu ya ku uwana kwa wingi, memu anaweza kuuwa mkewe ao kuuwa mume aliye mpenda mkewe, namzinifu kuuwa mume wa yule mke aliye mpenda, na mwanamke kuwa yule aliye zini naye, mfano ikiwa kazini naye kwa kumlazimisha.

Kwa hivyo vyote na vingine katika faida ya uislam kukataza zinaa na ika vijaaliya kuwa haramu, na ikawahalalishiya watu kuowana kupitiya katika familia na jamii.

### Kwa nini uislam ina haramisha uchawi?

Uchawi katika mtizamo wa sheria ya uislamu wote ni shari, na ndiyo maana sheria ya uislamu ina kataza na ina haramisha, ni kwa sababu lengo kubwa ya uchawi huwa ni kuleta mazara kati ya watu, na kuzua uadui baina yao, na mengi katika kazi wanazo zitumia wachawi haziingiye ispokuwa katika ulimwengu wa shari na kufanya ubaya kwa watu.

Na kinacho eleweka na ku kubalika hakika uislamu kuharamisha uchawi ni njiya ya kuvunja uchawi uwo, na kutakasa ulimwengu na watu kutokana na hiyo kazi mbaya yenye shari, naku takasa watu kutokana na uwongo na uzushi yenye kulingana nayo, na kutakasa jamii kutokana na uchawi na wachawi, na kufanya hivyo kuna faida kubua ya wazi.

islamu imeisha haramisha kutumikisha uchawi, na kwenda kwa wachawi na kuwaomba msaada, na kama vile iliharamisha kujifunza uchawi na kuyafundisha.

Hakika uchawi ni kugeuza ukweli, na kusambaza karaha, na kutangaza ubaya na kuzusha hali ya kuto kuaminiana katika jamii, na kutumiya njia ya uzhaifu wa watu na ujinga wao, ndiyo maana uislam inakataza na kuharamisha kwa ajili ya kumhifazi mtu na utukufu wake na heshima yake.

**Je! Uislamu unakubali udhihirisho wa ushirikina katika baadhi ya matendo ya ibada??**

Uislamu ni dini ya tauhid iliyotakasika kwa ajili yake Allah aliye takasika, na ndio mana haikuiachiya nafasi udhihirisho wowote katika udhihirishaji wa kumshirikisha Allah.

**Na shirki:** ni kumfanya Allah kuwa na mshirika katika Ubwana wake ao katika ibada ao katika Majina na Sifa zake.

Na katika kumshirikisha Allah ni kumfanyia yule asiye kuwa Allah haki zilizokuwa zake Allah katika ubwana wake na ibada zake na majina yake na sifa zake, mfano: kama ushirikina wa wale wanao abudu ma sanamu, wanao abudu makaburi na walio kufa na wale wasio kuwepo.

**Mfano :** kuitakidi kwamba kuna yule ana umba ao kuwapa watu uhai ao kifo, ao kuna yule ana miliki ao mwenye uwezo wa kufanya akitakacho kwenye ulimwengu huu pamoja na Allah.

**Ao mfano:** Kuitakidi kwamba kuna yule tunaweza kumtii utiifu wa bila mpaka pamoja na Allah, wanawatii katika kuhalilasha wanayo yataka na kuharamisha wanayo yataka hata kama hayo yanaenda kinyume na dini ya Mitume.

**Ao mfano:** kumshirikisha Allah katika mapenzi na kumtukuza, kama vile kumupenda mtu kama vile unampenda Allah, ao kuitakidi kwamba kuna anaye jua mambo ya siri pamoja na Allah.

Na haya ni miongoni mwa shirki ambayo allah mtukufu hawezi kuyasamehe siku ya qiyama, kasema Allah: {Hakika Allah hasamehe kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye, na anaye mshirikisha Allah basi hakika amezua dhambi kubwa} surat nisaa 48

Hakika ibada na ukamilifu wa kunyenyekeya na mapenzi kwa watu haiwezi kuwa ila kwa ajili tu ya Allah peke yake, wala haijuzu kwa mtu kubeba sehemu ata kidogo katika hilo.

Na hiyo ndiyo tofauti kubwa katika dini ya kiislamu, kwamba hakuna mwenye kuzuru ao kuleta manufaa wala kutegemewa wala wa kuabudiwa kwa haki ispokuwa tu Allah.

hatoweza yoyote katika viumbe kuleta mazuri ao mabaya kwa watu ispokuwa tu kwa uwezo wake Allah, na ndiyo maana Allah ka muamrisha Nabii wake kusema ndani ya qur'ani tukufu: {Sema: similiki nafsi yangu manufaa wala madhara, ila apendavyo Allah. Na lau kuwa ninayajua ya ghaibu(siri) ninge jizidishia mema mengi, wala ovu lisinge nigusa. Mimi si chochote ila ni mwonyaji na mbashiri kwa watu wanao amini} Surat a'raaf 188

Na yule atakaye mshirikisha Allah na vitu vingine, basi ameisha iangamiza nafsi yake, na haita mufaidisha kitu, kwa sababu dunia yote na viliomo ndani yake ni vya Allah, na viko chini ya ufalme na mamlaka yake Allah.

## Hitimisho

**Huu ni programu fupi inayo jumuisha hukumu za lazima za dini ya Kiislamu ili kumfundisha mwongofu mpya mambo muhimu anayopashwa kuyajua kuhusu hukumu za dini yake ya Kiislamu; Kwa hivyo, tuliacha kurefusha katika mada ambazo zilizo tajwa, ingawa mwongofu mpya anahitaji sana kuzijua, kama vile:**

1/ vipi uta ishi na familiya na jami ambayo inayo kuznguuka baada yakuwa muislamu.

2/ Iliyo kuwa halali  na haramu katika biashara na  ndoa na chakula na  vinywaji na mengine.

3/ kujibiya mada mbalimbali ambazo mwanafunzi mpya alikuwa akizitafutiya majibu kabla ya uislamu.

4/ kujua alama za kiyama, na vitisho vya siku ya hiyo, nasifa ya pepo, na sifa ya moto.

**Na kuhusiyana na hayo, inamlazimu yule ambaye ata somesha program iyi kwa waingiya dini wapya ni kwake:**

Kuandaa mihadhara minne au mitano au semina wakati wa wanafunzi wanasoma programu hii na ikijumuisha mada hizi zilizo ashiriwa.

kutenga muda wa kutosha kwa ajili ya kujibu maswali ya muislamu mpya na kuondoa mashaka yote, kama vile mwalimu anaweza akafanya hivyo, au kujisaidiza kwa baadhi ya wanafunzi waliopo ambao yawezekana kujisaidiza kwao.